Nipashe
Ijumaa Aprili 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580538
www.ippmedia.com
MWANGA WA
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Wanawake** walivyong'ara uteuzi wa mawaziri katika wizara nyeti

UKURASA 4



**Mwandishi** George Marato aachiwa huru kesi ya rushwa

UKURASA 8



**Madrid yampa Ramos mwaka**

UKURASA 21

# Rais Samia akonga nyoyo za walipakodi

• **Apiga** marufuku nguvu ukusanyaji mapato, kitendawili uteuzi makatibu wakuu ndani ya Pasaka...

*Endelea ukurasa 2&3*



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ndugai kicheko mawaziri kubaki

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

## ...Aonya makundi ya watu wanaosaka urais 2025

UKURASA 2

**MICHEZO** MANULA AIWEKA SIMBA MTEGONI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia akonga nyoyo za walipakodi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIKA kuhakikisha kauli yake ya mwanzo kwamba "hakitaharibika kitu" inatimia, Rais Samia Suluhu Hassan, ameibuka na faraja kwa wafanyabiashara, akionya utaratibu wa kudai kodi kwa nguvu kuwa unachangia kufunga biashara, hivyo kupunguza mapato ya serikali.

Rais Samia alitoa kauli hiyo ya kukonga nyoyo za walipakodi wakati wa hafla ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua juzi iliyofanyika Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma jana.

Aliweka wazi kwamba utaratibu unaotumika sasa katika kudai kodi kwa wafanyabiashara una ukakasi, akikemea kudai kodi kwa nguvu, kushikilia akaunti za benki za wafanyabiashara na kuchota fedha.

Rais Samia alisema ikiwa utaratibu huo utafumbiwa macho, wafanyabiashara wengi watafunga biashara zao nchini na kuhamishia uwekezaji wao kwenye nchi zingine. Alisema kuwa hilo likishafanyika, Tanzania itapoteza wafanyabiashara wengi na hivyo kurudi nyuma katika makusanyo ya kodi kutokana na walipakodi kupungua.

"Kwenye mapato na matumizi, Waziri wa Fedha (Dk. Mwigulu Nchemba), umepewa kigezo hapa cha kukusanya Sh. trilioni mbili kwa mwezi. Tunataka Sh. trilioni mbili kwa mwezi, muende mkatanue wigo wa kodi, lakini mtengeneze walipakodi wengi zaidi.

"Trend (mwenendo) mnaokwenda nao sasa hivi ni kuua walipakodi, mnaua wafanyabiashara, mnatumia nguvu zaidi kuliko akili na maarifa kupata kodi.

"Sasa wale mnaowakamua, mkienda mnachukua vifaa vyao vya kazi, mkienda mnafungia akaunti zao, mkachukua fedha kwa nguvu kwenye akaunti kisa sheria inakuruhusu ufanye hivyo, akitoka hapo, anakwenda kufunga biashara, anahamia nchi ya pili, mnapunguza walipakodi. "Ninaomba sana nendeni mkatengeneze, mkatanue wigo wa walipakodi. Mengine yanayopunguzia watu ari ya kulipa kodi, ninaomba mkayasimamie," Rais Samia aliagiza.

Alihitimisha kwa kudokeza kuwapo mabadiliko mengine ya uongozi akisema: "Tutamaliza pasaka Jumatatu, pengine Jumanne tutakuja kuapishana hapa (Ikulu Chamwino) na wengine. Ninawatakia kila la heri na Pasaka njema. Asanteni".

Kwa muda mrefu kumekuwa na kilio cha wafanyabiashara kuhusu utaratibu unaotumiwa na baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) katika kudai kodi na suala hilo limekuwa likiibua mijadala mikali ndani ya Bunge.



Balozi Hussein Athuman Katanga akila kiapo mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), kuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## ... Aonya makundi wasaka urais 2025

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameowaonya watendaji wa serikali, wakiwamo mawaziri, walioanza kujipanga kwa mbio za kuusaka urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Katika hotuba yake ya jana Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua juzi, Rais Samia alisema kuwa anawafuatilia kwa karibu watu hao.

Alisema rekodi za kiutendaji ndiyo zitaamua nani awe Rais wa Tanzania, akisisitiza kuwa atakuwa na umakini mkubwa katika mchakato wa kumpata kiongozi huyo.

"Ninafahamu 2025 iko karibu na kawaida yetu, sijui ni Watanzania tu au na kote ulimwenguni, kinapoingia kipindi cha pili cha Rais aliyepo madarakani, watu kidogo mnakuwa na lile na hili kuelekea mbele.

"Ninataka kuwaambia acheni. Twendeni tufanye kazi. Hili na lile tutajua mbele. Sawa ndugu zangu? Twendeni tufanye kazi. Rekodi yako inakufuata katika maisha yako.

"Kuna wengine wamekosa hizi nafasi kwa rekodi zao tu. Kwa hiyo, rekodi yako inakufuata kwenye maisha yako. Na mimi nitakuwa na jicho kubwa sana. Pamoja na kwamba (macho yangu) yamelegea, lakini yanaona.

"Nitakuwa na jicho kubwa sana kuangalia rekodi zenu na safari ya mbele yetu. Lakini ninataka kuwaambia, kila yule mwenye nia ya 2025, aache mara moja," Rais Samia alionya kwa msisitizo.

Aliwaonya mawaziri dhidi ya tabia za kujikweza, akisisitiza kuwa "nitakuwa na kipimo cha mabega. Nikiona mtu mabega yanazidi kupanda juu, ninajua huyu si mtumishi, huyo anafurahia juu ya kiti chake".

Alisema anatarajia kuona mawaziri wako mitaani wanatatua matatizo yanayowakabili wananchi, lakini ziara hizo zifanywe baada ya Bunge la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma.

Rais Samia pia aliwajibu wanaotaka aumalizie mchakato wa Tanzania kupata Katipa Mpya, akiwataka walisahau suala hilo kwa muda.

"Kwenye Bunge la Katiba... oh Bunge la Bajeti! Hivi nina maradhi gani na katiba? Ninadhani kwa sababu wamenisukuma sukuma sana, katiba... katiba... katiba... lakini wasahau kwanza kidogo.

"Kwenye Bunge la Bajeti, mawaziri wote wawapo bungeni. Mmoja akikwama hoja, mwengine anayejua anasimama kusaidia kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa. Wote tunatafuta bajeti ya serikali. Kwa hiyo mawaziri wote muwapo pale bungeni," aliagiza.

## Mrithi wa Bashiru afichua alivyopokea uteuzi akiwa 'airport'

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, amefichua akivyopokea taarifa za kuteuliwa kushika madaraka hayo wakati anajiandaa kwa safari ndefu ya kurejea Japan.

Kabla ya uteuzi huo uliofanywa juzi, Katanga alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Japan.

Baada ya kuapishwa jana kushika madaraka hayo mapya, Balozi Katanga alisema tayari alikuwa na tiketi ya ndege kurejea Japan, lakini wakati wa maandalizi ya mwisho ya safari yake hiyo, alifuatwa na maofisa waliomtaka kuondoka Dar es Salaam kwenda Ikulu, Dodoma.

"Waliniambia nikifika Dodoma, nitajua ninachoitiwa. Jioni wakati ninafuatilia TV, nikajua nilichoitiwa hata kabla ya kufika Dodoma," alisema na kufafanua namna safari yake ya kurejea kazini Japan ilivyositishwa.

Katanga alimshukuru Rais Samia kwa kumwamini kushika nafasi hiyo kubwa na kumwahidi kuwa atafanya kazi kwa mwongozo wa Mkuu wa Nchi huyo na miongozo mingine ya kikatiba.

Alisema anatambua kwamba shughuli za serikali zimegawanywa katika sekta mbalimbali, akiahidi kufanyia kazi dosari ya mpasuko wa kiutendaji iliyopo miongoni mwa watendaji wa serikali.

Awali, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alimtaka Balozi Katanga kufanyia kazi dosari hiyo kwa kuhakikisha kunakuwa na ushirikiano mzuri miongoni mwa watendaji wa serikali.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alimpongeza Balozi Katanga kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo, akikumbusha mambo mazuri aliyoyafanya akiwa mtumishi wa mahakama.

"Kwetu (mahakama) ukitaja jina la Katanga, unataja mabadiliko. Alifanya maboresho makubwa, alitubadilisha sana kiutumishi. Kwa kuwa alikuwa Japan, ninafikiri sasa mshindani awe Japan," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ndugai afurahia mawaziri kutoenguliwa



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UAMUZI wa Rais Samia Suluhu Hassan kutowaengua mawaziri walioteuliwa na mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli, umepongezwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai (pichani), huku akisisitiza kuwa 'huo ndio uzuri wa mama'. Spika Ndugai alitoa pongezi hizo bungeni jana baada ya kuwaapisha wabunge wapya walioteuliwa na Rais Samia juzi. Wabunge hao ni Balozi Dk. Bashiru Kakurwa, Balozi Liberata Mulamula na Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.

"Niwapongeze sana waheshimiwa mawaziri wetu na naibu mawaziri wote kwanza kwa kubaki kwenye baraza na huo ndio uzuri wa mama. Wangekuwa wenzetu wengine upewe panga hilo, majeruhi wangekuwa kibao. Lakini mama aah anapita salama katikati," alisema. Ndugai alisema Rais amewapa mawaziri dhamana ambayo inapaswa kufanyiwa kazi kwa dhamana ile ile ambayo amewapatia.

"Yapo mambo mengine ya kufanya kila mmoja kwenye wizara yake na mengi mtayapata kama ushauri kwa wabunge. La msingi waheshimiwa mawaziri ninyi ni wabunge kama sisi. Hilo ndilo la msingi, yaani hapa bungeni ndiyo nyumbani, huko mmeenda matembezi tu. Ikitokea kikirikakara mnarudi hapa hapa.

"Kwa hiyo tusisahauliane sana, yaani mtapata ushauri mwingi huko serikalini na kadhalika lakini msisahau kwamba ushauri wa wabunge ni muhimu kwa sababu ni ushauri wa wananchi kabisa kabisa," alisema.

Alibainisha kuwa kila wizara ina mambo ya msingi ya kushughulikia huku akitolea mfano wa malalamiko ya wafanyabiashara ambayo amekuwa akiyasikia kila siku.

"Hivi Waziri wa Uwekezaji; Viwanda na Biashara, Fedha na wanaoendana na kada ya biashara mnahitaji kengele gani igongwe kuwajulisha hili eneo ni kipaumbele namba moja?

"Waziri wa TAMISEMI ndio maendeleo ya mwananchi wa kawaida. Kule vijijini tunakoishi ndiyo anayegusa wananchi kule kabisa. Kale kadarasa kanachojengwa kuwatoa watoto kwenye mti sasa wanasoma kwenye darasa wanaacha kukaa chini sasa wanakaa kwenye kadawati, hii ni thawabu kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu.

"Pamoja na miradi mikubwa tunayofanya kielelezo na kadhalika, lakini TAMISEMI ile miradi midogo midogo kama zahanati, maji, darasa, barabara ni jambo la thawabu kubwa sana tusiwasahau watu hao," alisema.

Alisema suala la bima ya afya kwa Watanzania wote katika miaka mitano iliyopita halikufanikiwa.

Kuhusu sekta ya ardhi, Ndugai alisema: "Tumesema mara nyingi hapa tukiweza kuipima ardhi yetu yote mapato yanatokanayo na hati za ardhi yanaweza ku- double (kuongeza mara mbili) hii bajeti yetu. Kwa hiyo tuajiri wapima watu wapimiwe ardhi wawe na hati zao. Wenzetu wanaotamba wana bajeti kubwa fedha nyingi wanatoa kwenye ardhi kwa sababu ardhi imepimwa," alisema.

Akizungumzia mapumziko ya sikukuu ya Pasaka, Ndugai aliwashauri wabunge wanaosafiri kuwadhibiti madereva wao kuendesha kwa mwendokasi.

Hata hivyo, alisema kutokuwapo kwa kipindi cha maswali asubuhi ni kutokana na mabadiliko yaliyofanywa kwa mawaziri na watakapokabidhiana kipindi hicho kitaendelea.

# Mabadiliko makatibu wakuu yaja

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametangaza kufanya mabadiliko ya makatibu wakuu wa wizara huku akiwaonya wanaoendekeza migogoro na mivutano isiyo na tija.

Baada ya kuwaapisha Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana viongozi mbalimbali aliowateua juzi, Rais Samia alidokeza kusudio lake hilo la kufanya mabadiliko ya makatibu wakuu wa wizara.

Waliopaishwa ni Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, mawaziri na manaibu waziri, hafla ya kuapishwa kwao ikihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa.

"Makatibu wakuu mpo? Hallooooo! Siyo leo (jana), mmekuwa wanyonge, sauti hazitoki, siyo leo, lakini inakuja... Lazima jahazi likate mawimbi na safari ifike," alisema.

Alimtaka Balozi Katanga kuhakikisha ushirikiano wa kiutendaji miongoni mwa watendaji wa serikali unaimarishwa, akiweka wazi kwamba kwa sasa hali ni mbaya katika eneo hilo. "Huu ugonjwa uliouibua wakati unazungumza hapa ndiyo wenyewe na wewe ndio daktari wake. Kalishughulikie hilo ili kuwe na ushirikiano wa kiutendaji ndani ya serikali," aliagiza.

Rais Samia alitumia fursa hiyo kutaja sababu za kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, akibainisha kuwa amechukua mabingwa na wabobezi katika sekta husika na kuwapangia wizara husika pamoja na kuangalia sura ya Muungano, akiongeza wawili kutoka Zanzibar.

Rais Samia pia aliwakumbusha mawaziri kuwapangia kazi wasaidizi wao, akionya kuwa hatakuwa na huruma na atakayekiuka maagizo yake hayo.

Kabla Rais Samia kuonya kuhusu kukosekana kwa ushirikiano kiutendaji serikalini, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alidokeza kuwa dosari hiyo ni kubwa na imekuwa na madhara makubwa kiutendaji.

Alisema upo mvutano miongoni mwa mawaziri na manaibu waziri huku makatibu wakuu wakivutana na wasaidizi wao, yaani makatibu wakuu wasaidizi.


"Katibu mkuu msaidizi akifanya vizuri, inakuwa nongwa. Linakuwa tatizo kubwa hasa kwenye matumizi ya fedha. Ninawaambieni tutafuatilia huko. Ni muhimu kufanya kazi kama timu moja," aliagiza.

Dk. Mpango alisema wananchi wana matumaini makubwa na Rais Samia na 'amewakamata' ndani ya muda mfupi, hivyo wizara zote zinapaswa kushirikiana kuhakikisha zinaongeza makusanyo ya mapato.

Alimtaka mrithi wake katika Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuhakikisha serikali inakusanya wastani wa Sh. trilioni mbili kwa mwezi.

"Waziri Ummy (Mwalimu) pale TAMISEMI kuna kazi kubwa. Hakikisheni mnakusanya vizuri na kudhibiti matumizi ya fedha bila kupepesa macho.

"Nitafuatilia kwa karibu hili. Yeyote atakayeshindwa, nitakwenda kusema kwa mama 'huyu hatufai kukimbia na sisi'," Dk. Mpango alionya.




FARM AFRICA

**TENDER FOR WAREHOUSE CONSTRUCTION AT MNANG'ANA VILLAGE IN IKUNGI DISTRICT**

Farm Africa is a cutting-edge non-governmental organization delivering agriculture, natural resource management, and market system projects across eastern Africa. The organization works with key development actors, including smallholder farmers, pastoralists, communities, governments and the private sector to catalyze rural transformation in Africa. The organization has a deep commitment and long-term presence in the region, with over 25 years' experience of supporting rural communities in Tanzania to lift themselves out of poverty through interventions focused on improving production and productivity of crops, empowering communities to manage their natural resources sustainably, and increasing access to profitable markets.

**OUR MISSION:** We drive agricultural and environmental change to improve lives. Through our three strategic pillars of Agriculture, Market Engagement and Natural Resource Management, Farm Africa's mission is to help rural communities grow more, sell more and sell for more, while protecting the environment for years to come.

Farm Africa has been subcontracted by UN Women to implement a one-year project on "Realizing Gender Equality through Empowering Women and Adolescent Girls project" in Ikungi District of Singida Region.

Farm Africa now invites electronic priced tender from eligible civil contractors within Tanzania to construct a warehouse in at Mnang'ana Village in Ikungi District with capacity of storing 300 metric tonnes.

The detailed architecture design and other tender documents can be found and downloaded from Farm Africa website **https://www.farmafrica.org/tenders/tenders**.

Vendors must submit **electronic copies of their tenders through designated email tenderstanzania@farmafrica.org** addressed to the Country Director, Farm Africa Tanzania, with **clear email subject "Tender for Warehouse Construction".**

Deadline for receiving tender document is on Monday **19th, April 2021 at 12:00 noon EAT.**

# Wanawake walivyong'ara wizara nyeti

**Na Sanula Athanas**, DODOMA

JUZI Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri, huku wanawake wakizidi kuchomoza kwenye wizara nyeti.

Mabadiliko hayo ambayo ni hatua ya pili kwa Rais Samia katika kulisuka baraza lake baada ya kupendekeza jina la Makamu wa Rais na kupitishwa na Bunge, yanafanya idadi ya wizara zinazoongozwa na mawaziri wanawake kufika tano kutoka nne za awali kati ya wizara 23 zilizopo.

Wanawake hao watano wanaoongoza wizara nyeti ni pamoja na Ummy Mwalimu ambaye amehamishwa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwenda Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), akibadilishana wizara na Seleman Jafo aliyekaa kwa miaka sita katika wizara hiyo, akianzia kuwa naibu waziri.

Kwenye wizara hiyo, Ummy aliyefanya vizuri katika miaka mitano ya kwanza ya uongozi wa Hayati Rais John Magufuli akiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, atasaidiwa na Dk. Festo Dugange na David Silinde, ambao hawajahamishwa wizara.

Jenista Mhagama ameendelea kung'ara kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu akiendelea kusaidiwa na Patrobas Katambi na Ummy Nderianan ambao waliingia baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Mbobezi katika mitaala ya elimu, Profesa Joyce Ndalichako, ameendea kuaminiwa kuiongoza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, aliyoteuliwa tangu Hayati Rais Magufuli anaingia madarakani miaka sita iliyopita huku Naibu Waziri. Omar Kipanga, aliyeingia wizarani hapo mwaka jana naye akiendelea kuaminiwa.

Dk. Dorothy Gwajima aliyejizolea umaarufu mkubwa kutokana na kauli zake zilizojaa vijembe, amezidi kung'ara kwenye Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na safari hii ameongezwa nguvu na Rais Samia kwa kupewa Naibu Waziri wa pili, Mwanaidi Ali Khamis aliyehamishwa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, akiungana na Naibu Waziri mwingine, Dk. Godwin Mollel aliyeteuliwa na Hayati Rais Magufuli kuongoza wizara hiyo muda mfupi baada ya kuihama CHADEMA na kujiunga na CCM na kushinda uchaguzi mdogo wa Jimbo la Hai.

Nyota ya Balozi Liberata Mulamula imezidi kung'ara pale jicho la Rais Samia lilipomwona na kumteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, akichukua nafasi ya Profesa Palamagamba Kabudi aliyerudishwa kwenye Wizara ya Katiba na Sheria aliyoteuliwa kwa mara ya kwanza na Hayati Rais Magufuli baada ya aliyekuwa waziri wake kipindi hicho, Dk. Harrison Mwakyembe kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, akipishwa na Nape Nnauye aliyetumbuliwa.

Balozi Mulamula atasaidiwa na Mbarouk Nassor Mbarouk, aliyeteuliwa kuwa mbunge na naibu waziri juzi.

Mbali na hao, wanawake wengine ambao wameng'ara kwenye Baraza la Mawaziri wakiwa si mawaziri kamili ni pamoja na Dk. Angelina Mabula (Ardhi), MaryPrisca Mahundi (Maji), Mary Masanja (Utalii) na Pauline Gekul aliyehamishiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenda Wizara ya Habari.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama



Waziri ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima

Mbali na wanawake, mawaziri waliopenya kwenye mabadiliko ya Rais Samia ni pamoja na Mohammed Mchengerwa aliyeungana na Kapteni mstaafu George Mkuchika kwenye Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (lakini Mkuchika atapewa kazi maalum) wakisaidiwa na Deogratius Ndejembi.

Kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Jafo atasaidiwa na Hamad Hassan Chande, Mbunge wa Kojani mkoani Kaskazini Pemba.

Waziri Geoffrey Mwambe aliyekuwa Wizara ya Viwanda na Biashara kabla ya mabadiliko ya juzi, ataungana na William Ole Nasha katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji). Ole Nasha alikuwa Naibu Waziri wa Elimu katika miaka mitano ya mwanzo ya uongozi wa Hayati Rais Magufuli.

Kwenye Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu aliyehamishwa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, anaungana na Naibu Waziri Hamad Yussuf Masauni kuongoza wizara hiyo iliyoachwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na naibu wake, Mwanaidi.

Katika miaka mitano ya mwanzo ya uongozi wa Hayati Rais Magufuli, Dk. Mwigulu alishika wizara tatu akianzia Kilimo kisha Mambo ya Ndani ya Nchi ambako alitumbuliwa na baadaye kurejeshwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kufuatia kifo cha Balozi Dk. Augustine Mahiga. Katika miaka mitano hiyo, Masauni ambaye ameongeza idadi ya mawaziri kutoka Zanzibar kwenye Baraza la Rais Samia, alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, akipita chini ya mawaziri wanne: Charles Kitwanga; Dk. Mwigulu; Kangi Lugola; na George Simbachawene.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuwa chini ya Waziri Elias Kwandikwa huku Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikiongozwa na Simbachawene akisaidiwa na Khamis Hamza.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iko chini ya Waziri Leonard Chamriho na Naibu Waziri Geofrey Kasekenya na Mwita Waitara.

Wizara ya Viwanda na Biashara inaongozwa na Waziri Prof. Kitila Mkumbo aliyehamishiwa juzi kutoka Ofisi ya Rais - Uwekezaji na anasaidiwa na Naibu Waziri Exaud Kigahe.

Dotto Biteko ameendelea kuaminiwa katika Wizara ya Madini akisaidiwa na Naibu Waziri, Profesa Shukrani Manya huku William Lukuvi akizidi 'kupeta' kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Wizara ya Maji inaendelea kuwa chini ya Jumaa Aweso, huku Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ikiendelea kuongozwa na Innocent Bashungwa.

Wizara ya Nishati bado iko chini ya Dk. Medard Kalemani akisaidiwa na Stephen Byabato wakati Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea kuongozwa na mwanasheria na mhadhiri mzoefu, Dk. Damas Ndumbaro.

Prof. Adolf Mkenda anasaidiwa na Naibu Waziri Hussein Bashe katika Wizara ya Kilimo huku Mashimba Ndaki akiendelea kuaminiwa na Wizara wa Mifugo na Uvuvi, akisaidiwa na Abdallah, aliyehamishwa kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea kuwa chini ya Dk. Faustine Ndugulile anayesaidiwa na Naibu Waziri Kundo Mathew, huku Wizara ya Katiba na Sheria, ikirejeshwa kuwa chini ya Prof. Palamagamba Kabudi akisaidiana na Naibu Waziri Geofrey Pinda.

**SURA YA MUUNGANO**

Katika baraza hilo la Rais Samia, mawaziri kutoka Zanzibar na majimbo yao kwenye mabano ni: Mbarouk (Kuteuliwa na Rais); Mwanaidi (Viti Maalum); Masauni (Kikwajuni); Chande (Kojani, Pemba); na Hamza (Uzini).

## HABARI KITAIFA

# Polisi yapiga marufuku shamrashamra Pasaka

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limewahakikishia Watanzania ulinzi na usalama wakati wa Sikukuu ya Pasaka na kueleza kuwa halitegemei kuona shamrashamra zozote kwa sababu nchi bado iko kwenye kipindi cha maombolezo ya siku 21.

Msemaji wa Jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) David Misime, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Misime alisema Jeshi la Polisi limetoa maelekezo na mikakati kwa makamanda wa polisi wa mikoa watakayoitumia katika mazingira yao pamoja na ile waliyojipangia kupitia kamati za ulinzi na usalama ili ibada zimalizike salama.

"Tuna imani kila mwananchi atazingatia na kufuata sheria na kujiepusha na vishawishi vya kufanya vitendo vya uhalifu, ibada za Pasaka zitamalizika salama, tukizingatia kuwa bado tupo katika kipindi cha maombolezo.

"Hatutegemei sherehe na shamrashamra tulizozizoea kipindi cha miaka ya nyuma kuwapo katika kipindi hiki."

Misime alisema wakati nchi ikiendelea na maombolezo ya siku 21 baada ya kifo cha Rais John Magufuli, hadi sasa hali ya usalama ni shwari.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga vizuri kuhakikisha waumini wanafanya ibada kwa amani, utulivu na wananchi wengine kuendelea kufanya shughuli zao kama kawaida.

Kuhusu vyombo vya moto, jeshi hilo limewataka watumiaji wake kuhakikishe wanaviendesha kwa kufuata sheria za usalama barabarani ikiwamo kuepuka mwendo kasi na kunywa pombe.

Alisema utafiti uliofanyika unaonyesha asilimia 75 za ajali zinazotokea, husababishwa na uzembe wa binadamu.

# Serikali yapania kumaliza tatizo uhaba wa mbegu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imedhamiria kuzikutanisha Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA), Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ili kujadili na kuweka mkakati wa kitaalamu ili kukidhi mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (pichani), alisema hayo jana akielezea mikakati ya wizara ya uzalishaji wa mbegu akisema ili kufikia malengo hayo, fedha zote katika bajeti ya miradi mipya ya umwagiliaji itasimamishwa na zitaelekezwa kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu.

Prof. Mkenda alisema hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake, Dk. Christine Ishengoma iliyotembelea kukagua utendaji kazi wa ASA na TOSCI mjini hapa.

Alisema hatua hiyo inakusudia kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchini kwa ajili ya mahitaji ya wakulima na kuondokana kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi.

Waziri Mkenda alisema serikali imeweka kipaumbele kumaliza tatizo la mbegu, hivyo itashirikiana na kamati hiyo katika kulisukuma mbele ili kuona mbegu bora zinazalishwa kwa wingi.

"Sisi wizara tutaweka nguvu kwenye bajeti ili kuakisi vipaumbele vyake na kuiwezesha ASA ipate fedha za kutosha kwa ajili ya kusimamia majukumu yake kikamilifu ya kuzalisha na kusambaza mbegu bora nchini kote na kuhakikisha inaboresha mitambo yake.

"Pamoja na ASA pia tunakusudia kutaongeza fedha kwa TARI na usimamizi ili waongeze utafiti zaidi wa mbegu bora na kipaumbele kingine ni suala la ugani litaboreshwa zaidi," alisema Prof. Mkenda.



Alisema kazi kubwa zimefanyika kwa kuanza kupata mbegu bora nyingi kwa ajili ya wakulima na bajeti ya mwaka huu itaelekeza kwa Taasisi za uzalishaji wa Mbegu hasa ASA na TARI.

Takwimu zinaonyesha kwa kipindi cha miaka minne upatikanaji wa mbegu umeongezeka kutoka tani 36,614 mwaka 2015/16 hadi tani 76,725 mwaka 2019/20, huku uzalishaji wa ndani wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 20,604 mwaka 2015/16 hadi tani 69,173 mwaka 2019/20.

Naye Dk. Ishengoma alipongeza jitihada za Wizara ya Kilimo kuzalisha mbegu bora za mazao ya kilimo kupitia ASA.

Alisema tatizo la mbegu bora ni kubwa na kwamba serikali kupitia wizara hiyo inaweza kutatua changamoto hiyo kwa kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu na kuboresha shughuli za ugani.


TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

**PONGEZI**

**MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO**

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunakupongeza, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakutakia mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yako kwa maendeleo ya Taifa letu.




*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunatarajia mawaziri kuwatumikia Watanzania

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, alitangaza Baraza lake la Mawaziri na kuwaapisha jana, ambao sasa wana wajibu kumsaidia katika kuhakikisha kero za wananchi zinatatuliwa na kasi ya maendeleo inakuwapo.

Tunampongeza Rais Samia kwa uteuzi wake ambao umegusa maeneo mengi na mchanganyiko unaowakilisha kila kundi katika jamii na hasa kuwa na uwakilishi wa wastani wa wanawake.

Baada ya kukamilika kwa baraza hilo lenye sura ya tofauti na lililoteuliwa Desemba, mwaka jana, ikiwa watu ni wale wale na wapya wanne ambao sasa wanakwenda kutimiza wajibu wa msingi wa kuwatumikia wananchi katika maeneo (wizara) mapya huku wengine wakibakia pale pale. Matarajio ya Watanzania wengi ni kuona sasa uundaji wa serikali umekamilika na kazi ifanyike kwa muktadha wa kutatua kero za wananchi, nidhamu ya uwajibikaji serikalini na kupambana na rushwa ambayo ni saratani inayowaumiza wengi.

Kazi imeanza na sasa ni wakati wa kila kiongozi kuwajibika na kurekebisha pale ambako hakufanya vizuri kwa sababu fulani, hatutarajii kuona viongozi miungu watu, bali watu walioajiriwa na Watanzania ambao mishahara yao, marupurupu na huduma nyingi zote zinagharamiwa na waliowasababisha kuwa hapo.

Kama Mtanzania ndiye mwajiri basi ni lazima aliyeajiriwa apimwe kwa matokeo ya kazi anayoifanya, ili kuondoa ile dhana ya yeye kuwa bosi wa wananchi kiasi cha kuwafokea, kuwaumiza kwa vile tu ameshika madaraka. Kwa kutambua kuwa waajiri wao ni Watanzania sasa wakawatumikie vyema na mabadiliko makubwa katika huduma za afya kwamba kusiwe na majengo ya zahanati, vituo vya afya na hospitali bali kuwe na dawa na vifaa tiba.

Afya za Watanzania ni muhimu sana kwamba mtu anapokwenda hospitali apate huduma zote pamoja na dawa, pia tunatarajia kuona wote tunakuwa na Bima za Afya zinazoweza kutuhudumia vyema.

Maeneo mengine ni miundombinu mbalimbali kama ya maji kwamba ile ahadi ya kuhakikisha Mtanzania anapata maji umbali usiozidi mita 400, yakatimie ili kuondoa kero ya upatikanaji wa uhakika wa majisafi na salama.

Aidha, eneo jingine ni miundombinu ya elimu ya msingi hadi vyuo vikuu, kwamba pamoja na majengo mazuri basi kuwe na vitabu vya kiada na ziada. Matarajio yetu ni kuwa keki ya taifa itagawanywa kwa usawa kwa kuwa baraza hili limekuja wakati tayari Bunge la Bajeti limeanza ambalo litajadili na kupitisha bajeti ya serikali kwa mwaka 2021/22, ambayo ndiyo matazamio na matarajio makubwa ya Watanzania yapo humo. Haitarajiwi kuona mawaziri wakatumia nafasi zao kujilimbikizia mali au kuwa sehemu ya rushwa kwenye taasisi zilizopo chini yao, ni muhimu sana kila mmoja akawajibika ipasavyo kwa nafasi yake ili kufikia matazamio.

Mawaziri wamesikika wakionyesha uchungu dhidi ya wale waliowaita wanyonge na maskini, basi kama ndivyo wameajiriwa na watu hao, na hao wavuja jasho ndio wanaojinyima na kuhakikisha wanaishi vizuri na familia zao, sasa tuone hali za maisha za waajiri (Watanzania) zinaboreka. Mathalani kwa sasa kuna utitiri wa kodi na mchakato mrefu wa kuanzisha na kusajili biashara, kuna kasi ya kufunga biashara za watu walioshindwa kulipa kodi, pamoja na kufunga akaunti za watu kiasi cha kusababisha wengi badala ya kuendelea kukusanya kidogo na kulipa kodi sasa wamefunga au kufa.

Kama idadi kubwa ya watu itaendelea kuwa mtaani bila ajira anayeumia siyo mtu, bali serikali kwa ujumla kwa kuwa itakosa mapato ambayo yangetumika kupeleka huduma muhimu kwa jamii.

Matarajio makubwa ni serikali za mitaa ambako huko kuna saratani sugu ya matumizi sahihi ya fedha za umma, huko ndiko fedha nyingi hupelekwa na kunagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, lazima kusimamiwe vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani ukoma na kifua kikuu vina hatari, vilevile yanazuilika



Na Sabato Kasika

**MNAMO** Machi 24, mwaka huu, kama ilivyo kila mwaka Watanzania wanaadhimisha Siku ya Kifua Kikuu na Ukoma Duniani. Sisi Watanzania huwa tunaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku hiyo.

Kifua kikuu au maarufu 'TB' kinatajwa kuwa miongoni mwa magonjwa ambayo yanawakumba watu wengi maskini na kwamba, wanaoathirika kwa kiasi kikubwa, ni wale wanaotoka katika nchi zinazoendelea.

Inaelezwa na wataalamu wa afya, kwamba kuna aina kuu tatu za kifua kikuu, kikiwamo ambacho hutokea pale ambapo bakteria waliopo mwilini wapo hai na kinga ya mwili imeshindwa kuwadhibiti wasisababishe madhara.

Katika ufafanuzi wake, Daktari Bingwa, Mhadhiri wa Chuo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma na Mtaalamu wa Tiba na Uchunguzi kwa kutumia mionzi ya nyuklia Dk. Khamis Bakari, anaorodhesha namna kadhaa TB inavyoambaa.

Hapo anataja njia ya kuvuta pumzi na kukohoa, kutema mate, kupiga chafya, kupiga kelele iwapo watafanya vitendo hivyo karibu na watu wasio na ugonjwa huo.

Aina nyingine ya ugonjwa huo, inatajwa ni ile isiyo na madhara, kitaalamu wakiita 'latent TB' na huwa kwamba, anayeumwa huwa hajihisi na hawezi kumwambukiza mwingine.

Shida yake ni kwamba, aina hiyo inaweza kujirudia na kuathiri sehemu ya juu ya mapafu na kusababisha kikohozi cha kawaida, ambacho baadaye huongezeka na kusababisha mtu kukohoa damu au makohozi.

Vilevile, kuna suala la mtu kuugua homa, kupungukiwa hamu ya kula, kupungua uzito bila sababu ya msingi na wakati mwingine mtu anaweza kutokwa na jasho kwa wingi kuliko kawaida na hasa usiku.

Aina ya tatu ya kifua kikuu, inatajwa kuwa ni ule uliosambaa mwilini na kwamba hiyo hutokea pale ambao kinga ya mwili imepungua na kusababisha ugonjwa huo kuenea, kupitia damu hadi sehemu nyingine za mwili.

Sehemu hizo za mwili ni mifupa, mishipa ya fahamu, ngozi, figo, kibofu cha mkojo, ngozi ya moyo (pericadium), mfumo wa uzazi, viunganishi vya mifupa (joints) na mfumo wa mifupa na mishipa ulivyo.

Mbali na aina hiyo ya kifua kikuu, mtaalamu wa afya, anataja baadhi ya vihatarishi vya ugonjwa huo kuwa ni kuzeeka unywaji pombe kupindukia na kuishi sehemu zenye mrundikano wa watu.

Wataalamu wa afya wanapotoa ushauri huo wa jinsi ya kujikinga na kifua kikuu, kinachobaki na sisi wenyewe kuuzingatia, ili kuepuka kuambukiza au kuambukizwa kifua kikuu.

Pamoja na kwamba inawezekana huo ni ugonjwa wa kudumu katika nchi zinazoendelea, kifua kikuu kinazuilika iwapo kila mmoja wetu atafuata na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.

Iko hivyo, kwa sababu zaidi ya watu 4,000 wanakufa kwa kifua kikuu kila siku duniani, huku wengine karibu milioni 10 wakiambukizwa ugonjwa huo kila mwaka duniani.

Wakati idadi hiyo ikitajwa kuambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu, ajabu ni kwamba, wanajitokeza watu wachache kwa ajili ya kupata dawa muhimu za kuokoa maisha yao.

Katika maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani mwaka jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus, anatoa taarifa hiyo na kusema, ugonjwa huo unaathiri mapafu na kusababisha mtu kuwa hatarini.

Wakati kukiwa na taarifa iliotolewa na shirika hilo, Tanzania inazidi kuendelea kupiga hatua katika kupunguza kasi ya maambukizo mapya ya ugonjwa wa kifua kikuu kwa asilimia 18 kwa mwaka 2020.

Ripoti ya shirika hilo inasemwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika kilele cha kupokea taarifa ya tathmini ya mpango mkakati wa tano wa kati ya mwaka 2015-2020, kuhusu kifua kikuu na ukoma.

Hadi kufikia mwaka jana, wizara inaeleza kuwa iliongeza uwezo wa ugunduzi na kuibua wagonjwa wengi zaidi kutoka asilimia 29 mwaka 2015 hadi asilimia 53 mwaka jana na kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi saba duniani zilizofikia malengo hayo ya mwaka 2020 ya kupunguza maambukizo mapya.

Inaelezwa kuwa mwaka jana, wamegunduliwa wagonjwa karibia 82,140 na kadri inavyogunduliwa, ndivyo serikali inajitahidi kudhibiti maambukizi.

HABARI KITAIFA

# Madereva 10 wa mabasi wafungiwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene amewafungia kwa muda wa miezi mitatu madereva 10 wa mabasi ambao wamekuwa wakikiuka sheria ya usalama barabarani kwa kuendesha kwa mwendo wa kasi vyombo vya usafiri.

Aidha, ameliagiza Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuwachukulia hatua madereva hao ikiwamo kuwapeleka mahakamani kwa makosa hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Simbachawene aliwataja madereva hao ni Allan Msangi ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T605 DJR kutoka Kampuni ya Kapricon ambalo hufanya safari zake katika mikoa ya Dar es Salaam na Kilimanjaro na hutembea kwa kilomita 125 kwa saa.

Waziri huyo alimtaja dereva mwingine ni Hussein Dudu kutoka kampuni ya Kimotco Intertrade, ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T520 CXE, ambalo hufanya safari Arusha-Musoma na hutumia mwendokasi wa kilomita 126 kwa saa.

Mwingine ni Selemani Selemani, ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 313 DSO kutoka kampuni ya Al Saedy ambalo hufanya safari zake katika njia ya Dar es Salaam-Kilombero na hutumia mwendokasi wa kilomita 103 kwa saa.

Alimtaja dereva mwingine ni Athumani Mzava ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 391 kutoka kampuni ya MB Coach ambalo hufanya safari zake katika njia ya Dar es Salaam-Arusha na hutumia mwendokasi wa kilomita 107 kwa saa.

Waziri Simbachawene alimtaja dereva mwingine ni Juma Simba, ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 340 DPW kutoka Kampuni ya Baraka Classic ambalo hufanya safari zake katika maeneo ya Dar es Salaam- Masasi na hutumia mwendokasi wa kilomita 107 kwa saa.

Dereva mwingine aliyesimamishwa ni Salum Salum ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 121 DEA kutoka Kampuni ya Maning Nice ambalo hufanya safari zake Dar es Salaam - Tunduma na hutumia mwendokasi wa kilomita 110 kwa saa.

Mwingine ni Frank Masawe, ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 694 DRB kutoka kampuni ya Machinga ambalo hufanya safari zake katika Mikoa ya Dar es Salaam - Mtwara na hutumia mwendokasi wa kilomita 95 kwa saa.

Pia alimtaja dereva mwingine kuwa ni Innocent Thomas ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 225DTB kutoka kampuni ya Ester Luxury ambalo hufanya safari zake katika mikoa ya Dar es Salaam-Moshi na hutumia mwendokasi wa kilomita 107 kwa saa.

Kadhalika, Waziri Simbachawene alisema dereva mwingine ni Nassib Nasoro ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 565 BED kutoka kampuni ya NBS Classic ambalo hufanya safari zake katika mikoa ya Tabora na Kigoma na hutumia mwendokasi wa kilomita 109 kwa saa.

Vile vile, alimtaja dereva mwingine ni Maiko Mkindi ambaye huendesha gari lenye namba za usajili T 675 DHY kutoka kampuni ya Kilimanjaro Express ambalo hufanya safari zake katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha na hutumia mwendokasi wa km 100 kwa saa.

"Kwa mamlaka niliyonayo nawafungia madereva hawa kwa muda wa miezi mitatu nawaagiza wamiliki wa mabasi haya ambayo madereva wamekiuka sheria ya usalama barabarani kuhakikisha wanachukua hatua stahiki kwa madereva wao," alisema Simbachawene.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa linawapeleka mahakamani madereva hao ili iwe fundisho kwa wengine.

# Wanafunzi 300 wasomea katika darasa moja

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wanafunzi 300 wa Shule ya Msingi Kabale, Kata ya Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wanasoma katika chumba kimoja kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Shule hiyo ina ya wanafunzi 1,826 huku vyumba vya madarasa vikiwa vinane kati ya 40 vinavyohitajika. Pia chumba kimoja kinatumika kama ofisi ya walimu, ofisi ya mwalimu mkuu, stoo na maktaba.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Elias Kihamba, aliyabainisha hayo jana wakati akipokea mifuko 25 ya saruji kati ya 50 iliyotolewa na Kampuni ya Saruji ya Lake inayotengeneza saruji chapa Nyati, ikiwa jitihada za kuendelea kusaidia kutatua ukosefu wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari wilayani Kahama.

Alisema chumba kimoja kinatumiwa na wanafunzi 300 hadi 350 huku walimu wakipata changamoto ya kufundisha. Idadi inayotakiwa kisheria ni wanafunzi 40 hadi 45 kwa darasa moja.

Alisema katika shule hiyo imekuwa na tofauti na kusababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kuelewa kinachofundishwa.

"Darasa la kwanza na pili wanasoma kwa zamu na wale wa awali wanasoma nje ya darasa huku madarasa mengine yaliyobaki wakisomea darasa moja. Pamoja na shule hii kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi, bado imekuwa ikiongoza katika matokeo ya darasa la nne katika Halmashauri ya Msalala, " alisema Kihamba.

Akikabidhi saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, Ofisa Masoko wa Lake Cement Kanda ya Ziwa, Fadhiri Yustace, alisema kampuni yake imetoa mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni moja ili kuunga mkono serikali katika maendeleo hasa sekta ya elimu.

Akipokea saruji hiyo, Macha alisema itaelekezwa katika Shule ya Msingi Nyahanga iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Kabale katika Halmashauri ya Msalala.



## Wafanyabiashara wamwangukia Samia Suluhu

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WAFANYABIASHA wadogo wilayani Bagamoyo, wamemwomba Rais Samia Suluhu kutafuta ufumbuzi wa kodi wanazolipa ambazo wamesema zimekuwa kikwazo na kusababisha baadhi yao kufunga biashara.

Wakizungumza jana kuhusu kero hiyo mjini hapa, walisema idadi kubwa ya wafanyabiashara wamefunga maduka kutokana na kodi kutokuwa rafiki kwao.

Mwajuma Juma, aliiomba serikali kufanyia kazi kero hiyo huku akibainisha kuwa kodi kubwa wanayotozwa baadhi ya wafanyabiashara ni tofauti na biashara wanazozifanya hali inayosababisha kushindwa kumudu kuzilipa na kuamua kufunga maduka.

Mwakuma alisema wanampongeza Rais Samia na wanaimani na uongozi wake utashughulikia kero za wananchi wanaopambana kujikwamua kiuchumi.

Naye Mohamed Farsy alisema kwamba wengi wao wamefunga maduka kutokana na kushindwa kulipa kodi za majengo na za biashara.

Abeid Ally alisema pamoja na kwamba ulipaji wa kodi ndio nguzo katika nchi yoyote, wameomba iwe rafiki ili wengi wafungue maduka na kuendeleza biashara zao.

# 'Hayati Magufuli aliipaisha sekta uvuvi'

**Na Mbaraka Kambona**

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema utashi wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli wa kuamua kuwekeza katika sekta ya uvuvi umechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta hiyo.

Dk. Tamatamah alisema hayo alipokuwa akifungua warsha ya uzinduzi wa mpango kazi wa kutekeleza mwongozo wa hiari wa uendelezaji wa uvuvi mdogo nchini inayofanyika mkoani Morogoro kuanzia Machi 30-31, 2021. Akiongea na wadau wa sekta hiyo, Dk. Tamatamah alisema utayari wa hayati Dk. Magufuli kuwekeza katika sekta ya uvuvi umesababisha kuanzishwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Sisi ambao tupo katika ngazi za juu za wizara tunatambua kwamba utayari wake wa kuona kwamba mchango wa sekta ya uvuvi unakuwa mkubwa katika pato la taifa umepelekea mipango mikubwa ya uwekezaji ambayo itatekelezwa wizarani katika mwaka ujao wa fedha," alisema.

Pia alisema utayari wake wa kununua meli nane za kufanya uvuvi katika bahari kuu ulisababisha timu ya wataalamu wa serikali iliyokuwa kwenye majadiliano na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), kuhusu mkopo wa kuendeleza sekta ya uvuvi waweke kipaumbele ununuzi wa meli hizo miongoni mwa vitu vitakavyofadhiliwa na mradi huo.

"Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, serikali itatumia kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya kwanza ya uvuvi ambao utafanyika katika eneo la Mbegani Bagamoyo, hizi zote ni juhudi na msukumo wake," alifafanua Dk. Tamatamah.

Alisema pamoja na nchi kupata msiba huo, uongozi uliopo sasa chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, hakuna shaka kuwa mipango yote ya uwekezaji iliyoachwa na Hayati, Dk. Magufuli katika sekta hiyo itatekelezwa kama ilivyopangwa ili kutimiza malengo yaliyowekwa katika utawala wake.

Kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo Nchini, Dk. Tamatamah alisema kuzinduliwa kwa mpango huo kutakuwa ni ukombozi kwa wavuvi wadogo kwa sababu umeonyesha njia bora zitakazowezesha hali ya wavuvi wadogo kuimarika na kuinua uchumi wao.

"Mpango huu utasaidia wavuvi wadogo kufanya uvuvi endelevu ikiwamo kusimamia rasilimali za uvuvi katika muktadha wa chakula na kuondoa umaskini," alisema Dk. Tamatamah.

Kwa upande wa wadau, Katibu wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi cha Rasilimali za Bahari (BMU), Kilindoni, Wilayani Mafia alisema kuwa wanaishukuru serikali kutambua mchango wa wavuvi wadogo na kuamua kuandaa mpango huo ambao utawasaidia kupata masoko ya uhakika na zana bora za uvuvi kwa ajili ya uvuvi endelevu.

Naye Suzana Ezekiel, mvuvi mdogo anayefanya shughuli zake katika Mwalo wa Kibirizi, Kigoma alisema kuwa wavuvi wengi wadogo bado wanafanya shughuli zao kwa kubahatisha, lakini Mpango kazi huo utawawezesha kuondokana na hali hiyo na kufanya uvuvi endelevu na wa uhakika.



Mfanyabiashara wa maboga akiwa amejipumzisha wakati akisubiri wateja katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yamwachia huru mwandishi George Marato

**Na Robinson Wangaso,** MUSOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Musoma, mkoani Mara imemwachia huru aliyekuwa mwandishi wa habari mwandamizi wa ITV/ Radio One, mkoani Mara, George Marato, baada ya kutopatikana na hatia dhidi ya kesi ya tuhuma za kushawishi na kupewa rushwa.

Katika hukumu hiyo mshtakiwa mwenzake Lubango Mleka, aliyekuwa askari polisi, amekutwa na hatia ya kushawishi na kupewa shilingi milioni tatu.

Akisoma hukumu hiyo Machi 31, katika Mahakama ya Wilaya ya Musoma, Hakimu Tumaini James Marwa, alisema pamoja na upande wa Jamhuri kuleta mahakamani hapo mashahidi 10, wote hawakutoa ushahidi wa kumtia hatiani mshtakiwa namba moja Marato.

"Mahakama ilijiridhisha kuwa Marato aliingia katika mnyonyoro huo baada ya kuombwa na mlalamikaji, Wambura Chegere, mfanyabiashara wa duka barabara ya Majita, Manispaa ya Musoma kuongozana naye kama mdhamini katika tuhuma za kesi ya mauaji yaliyofanyika katika kata ya Bweri," alisema.

Hakimu Marwa alisema watu hao walishtakiwa kwa kifungu cha Sheria ya Makosa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 15 kifungu kidogo cha 1 A na B na kifungu cha pili kwamba walituhumiwa kwa kumshawishi mfanyabiashara huyo awalipe kiasi hicho cha fedha ili wamsaidie kumwondoa katika orodha ya watuhumiwa wa kesi hiyo ya mauaji ambayo Wambura akiwa ni miongoni mwa watuhumiwa.

Hakimu alisema mahakama ilijiridhisha kuwa mtuhumiwa namba mbili, Lubango Mleka, akiwa askari wa Jeshi la Polisi akihudumu katika ofisi ya Kamanda wa Mkoa wa Mara, alimwita mara kadhaa mfanyabiashara huyo katika ofisi ya kamanda na kumhoji kuhusika katika tukio la mauaji, mazingira ambayo hayakuwa sahihi kwa mtuhumiwa kuitwa na hivyo mahakama kumkuta na hatia na kumhukumu kulipa faini ya Sh. 500,000 au kifungo gerezani cha miaka mitatu. mshtakiwa alilipa faini hiyo na kuachiwa huru.

Kwa upande wa Jamhuri ambaye ni mlalamikaji, uliwakilishwa na Wakili Mashal Mseja, ambaye alisema uamuzi wa kuachiwa unatokana na upande huo kutokuwa na kumbukumbu za mshtakiwa kufanya kosa kama hilo kwa siku za nyuma huku upande wa utetezi washtakiwa wakijitetea wenyewe.

Alipotakiwa kujitetea baada ya kupatikana na hatia, mshtakiwa namba mbili, Lubango Mleka, aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kutokana na kuwa na majukumu ya familia inayomtegemea na kwa muda mrefu tangu mwaka 2019 aliposimamishwa kazi katika Jeshi la Polisi.

Kwa upande wake Marato akizungumzia hukumu hiyo, alipongeza uamuzi wa mahakama kwa kutenda haki dhidi yake na ameridhika na hukumu iliyotolewa.

HABARI KITAIFA

## Wateja wa Tigo Pesa kurahisishiwa miamala

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imetangaza rasmi ushirikiano wake na kampuni ya Visa Inc. utakaowezesha wateja kufanya miamala kwa urahisi zaidi, kutoka benki kwenda kwenye akaunti zao za Tigo Pesa kwa kutumia huduma ya Visa Direct.

Visa Direct ni huduma ya malipo ya kidigitali inayowezesha malipo ya ndani na nje ya nchi kwa haraka na usalama zaidi.

Ikipewa nguvu na mshirika wa Tigo, Business Connexion Tanzania Ltd (BCX) huduma hii inawawezesha wateja milioni 9 kutumia huduma za kifedha ya Tigo Pesa kutuma pesa kutoka kwenye akaunti ya benki kwenda kwenye akaunti ya Tigo Pesa haraka na kwa usalama.

Wateja wa Tigo wanaweza kuunganisha Kadi za Visa kwa kutumia simu janja kwenye App ya Tigo Pesa au Tigo Pesa USSD *150*01#. Mara baada ya kadi kuunganishwa taarifa zitatunzwa kwa usalama na mteja ataweza kufanya miamala papo hapo kwa kutumia App ya Tigo Pesa au menyu ya *150*01# kutoka kwenye kadi zao za Visa kwenda kwenye akaunti za Tigo Pesa moja kwa moja. "Hii inawapa wateja wetu uhuru zaidi wa kufanya miamala kwa haraka kutoka benki, pia itaongeza ufanyaji wa miamala kidigitali kwa kuondoa haja ya kwenda katika ATM kutoa pesa na baadaye kuingiza kwenye akaunti ya Tigo Pesa. Kwa huduma hii miamala itafanyika moja kwa moja kwenye mfumo wa Tigo Pesa kwa njia ya App au Menyu (USSD) na kufurahia maisha ya kidigitali kupitia mtandao mkubwa wa 4G, nyingine ya kwanza Tanzania na ya kwanza kutoka Tigo Pesa," alisema Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha.

Pesha alisema ushirikiano huo unadhihirisha nafasi yao kama mtoa huduma wa huduma za kifedha Tanzania na ni imani yao kuwa kuwa muungano huo utaongeza imani kwa wateja, idadi ya miamala na kufungua nafasi za ubia siku zijazo.

"Tigo ipo kidete kuhakikisha inachochea maisha ya kidigitali kwa kupitia Tigo Pesa ikiongoza katika ubunifu katika huduma za kifedha kwa simu kwa kuwa ya kwanza kuwezesha kufanya miamala kupitia Visa kwenda akaunti za simu. Hii inaonesha Tigo Pesa ni huduma kamili ya kifedha ikiwapa wateja huduma bora zaidi za kidigitali," aliongeza Pesha.

"Iwe kutuma pesa kwa familia nje ya nchi au kupata pesa papo hapo, huduma ya haraka na usalama ni muhimu hasa kipindi hiki cha Covid-19. Ushirikiano wetu kati ya Visa na Tigo Pesa unawapa uwezo wateja kunufaika na uhakika na usalama kupitia Visa ambayo inatumika na wateja bilioni 3 duniani," alisema Corine Mbiaketcha, Makamu wa Rais na Meneja Mkuu wa Visa-Afrika Mashariki.

# Dar yashauriwa bajeti ya mrengo wa kijinsia

**Na Sabato Kasika**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam imetakiwa kutenga bajeti yenye mrengo wa kijinsia, ili kuwapunguzia wanawake na wasichana kero mbalimbali zinazowakabili kwenye huduma za kijamii.

Wito huo ulitolewa na mwezeshaji kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gemma Akilimali, wakati akiendesha semina kujenga uelewa wa umuhimu wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa wakuu wa idara wa jiji hilo.

Mwezeshaji huyo alilenga bejeti ya mwaka 2021/2022, na kutaka izingatie mrengo wa kijinsia na kwamba, kutozingatia hilo husababisha kero katika huduma za kijamii zikiwamo za afya, maji na nyingine nyingi.

"Bajeti yenye mrengo wa kijinsia inazingatia upatikanaji wa fedha, mgawanyo wake na mahitaji gani yaliyopo na nani yanamgusa zaidi, jamii inahitaji afya, shule, maji na huduma nyingine muhimu," alisema Gemma.

Alisema, katika huduma hizo, mahitaji ya wanawake ni mengi zaidi kuliko wanaume, na kwamba bajeti ikizingatia mahitaji ya wengi, itakuwa ni rahisi kupunguza kero zinazowakabili wanawake.

"Kwa mfano katika shule, wanafunzi wa kike wanatakiwa kuwa na matundu ya vyoo ya kutosha, lakini na chumba maalum cha kujihifadhia, kuwa na taulo za kike na vilevile shule kuwa na maji ya kutosha," alisema.

Kaimu Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Beata Ezekia, alisema, watafanyia kazi mafunzo hayo kwenye bajeti ya mwaka 2022, 2023, kwa madai kwamba ya mwaka huu imeshaandaliwa.

Alisema, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ina idara 13 na kwamba kila mmoja huwa inaangalia vipaumbele vinavyolenga kuwaondolea wananchi kero mbalimbali zinazowakabili.

Kwa niaba ya Ofisa Elimu Jiji la Dar es Salaam, Ofisa Taalum wa jiji hilo, Doreen Massawe, alisema, wamekuwa wakijitahidi watoto wa kike wanapata mahitaji yao muhimu wawapo shuleni.

Mhandisi wa jiji hilo, John Magori, alisema wao wanajitahidi kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo ya barabara na hata kuweka taa za sola, lakini bahati mbaya baadhi ya watu wanaiba sola hizo.

"Serikali inatumia fedha nyingi kujenga na kuboresha miundombinu, lakini kinyume chake, baadhi ya watu wanaiharibu ikiwamo kuiba sola, nadhani umefika wakati kwa jamii kubadilika," alisema Mhandisi Magori.




Mafundi wakiendelea na kazi ya kuondoa lami ya zamani na kuweka mpya katika eneo la Mburahati Mianzini, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: MIRAJI MSALA

# Shinyanga yatishiwa jangwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KUSUA kwa upandaji miti, ukataji, na uchomaji wa mikaa ovyo mkoani Shinyanga, imetajwa kuwa chanzo cha mkoa huo kukabiliwa na hali ya jangwa.

Imeelezwa miaka ya nyuma Mkoa wa Shinyanga ulikuwa umefanikiwa na misitu, lakini baada ya kukithiri kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo uchomaji wa mikaa, miti mingi imekatwa, huku upandaji wake ukisuasua na kusababisha kuanza kukabiliwa na hali ya jangwa.

Perfect Mbwambo, Kaimu Ofisa Misitu na Mazingira Mkoa wa Shinyanga, alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa hali ya uharibifu wa mazingira mkoani humo ni kubwa, huku mwitikio wa upandaji miti ukiwa mdogo na kusababisha kushindwa kufikia malengo ya kuifanya Shinyanga kuwa ya kijani.

Alisema Mkoa wa Shinyanga una halmashauri sita, na kila halmashauri imewekewa lengo la kila mwaka kupanda miti milioni 1.5, lakini mwitikio wake ni mdogo kutokana na suala hilo kutopewa kipaumbele, huku wakishindwa pia kusimamia sheria za kuzuia ukataji miti hivyo, na kuufanya mkoa kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Shinyanga ni mkubwa sana, kutokana na asilimia 90 ya wananchi wanategemea kutumia nishati ya misitu kupikia chakula na kusababisha ukataji wa miti ovyo, na kuufanya mkoa kukabiliwa na hali ya jangwa," alisema Mbwambo.

Pia alitaja takwimu za upandaji miti kwa kila halmashauri ya mkoa huo kwa (2019-2020), ambapo mwaka huu halmashauri iliyopeleka takwimu ni Kishapu pekee, na kubainisha Manispaa ya Kahama ilikuwa na lengo la kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka, lakini wamepanda miti 14,000.

Mbwambo alitaja takwimu za halmashauri zingine kuwa Kishapu kati ya upandaji miti milioni 1.5 wamepanda miti 160,180, Msalala 191,250, Ushetu 565,979, Shinyanga Manispaa 283,115, na Wilaya ya Shinyanga miti iliyopandwa ni 79,000 na kubainisha kuwa hali hiyo ya upandaji miti siyo ya kuridhisha ili kuifanya Shinyanga kuwa ya kijani.

# Taasisi yataka vikwazo kwa watoto wa kike kuondolewa

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Usomaji kwa Maarifa na Maendeleo (SOMA), imesema bado kuna changamoto kubwa zinazowakwamisha watoto wa kike kufikia ndoto zao kielimu.

Akizungumza wakati wa kumtambua msichana, Gwantwa Lucas aliyebuni programu inayoelimisha jamii juu ya vikwazo anavyokutana navyo mtoto wa kike katika kufikia ndoto zake kielimu, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo ya SOMA, Demere Kitunga, alisema bado jamii ina uelewa potofu kuhusu maendeleo ya kielimu kwa mtoto wa kike.

Alisema bado jamii inaamini kwamba mtoto wa kike aliyesoma sana hawezi kuolewa kiurahisi.

Alisema baadhi ya watoto wa kike wamekuwa wakikwama kufikia ndoto zao kielimu hususani katika elimu ya juu kwa kuhofia kushindwa kuolewa.

"Bado kuna mtazamo mbovu kwenye jamii, wanaamini kwamba endapo mtoto wa kike akisoma zaidi hadi kufikia shahada ya uzamili au na kuendelea kabla hajaolewa, hawezi kuolewa tena baada ya hapo au atapata taabu kumpata mwanaume wa kumuoa," alisema Kitunga.

"Na hii imebainika pia hata kwa baadhi ya wazazi, kuwaambia watoto wao waolewe kwanza kabla ya kufikia mbali zaidi katika safari yao kielimu ili baadaye wasije wakashindwa kuolewa. Huu ni mtazamo hasi na unatakiwa kupigwa vita kwenye jamii yetu."

"Mtoto wa kike anaposoma zaidi ndipo anajiweka katika nafasi nzuri zaidi iwe katika kuendesha maisha yake na mengine yote hususani katika nyakati hizi za sayansi na teknolojia, kwa hiyo ni vema watoto wa kike wakaachwa watimize ndoto zao za kusoma watakavyo na si kuwawekea vikwazo kwa fikra ambazo siyo sahihi."

Alisema bado juhudi kubwa zinahitajika katika kupambana na vikwazo mbalimbali vinavyowakabili watoto hao wa kike katika kufikia ndoto zao kielimu.

"Ingawa kuna maendeleo ambayo yameanza kuonekana katika kutimiza haki za wasichana wadogo, lakini bado juhudi kubwa zaidi zinahitajika katika kupambana na changamoto mpya zinazojitokeza katika kuwakwamisha," alisema Kitunga.

Kwa upande wake msichana huyo aliyebuni mpango wa kutambua vikwazo kwa watoto wa kike, Gwantwa Lucas, alisema mradi wake huo ambao ni wa majaribio na unalenga kuelezea vikwazo mbalimbali anavyokumbana navyo mtoto wa kike pamoja na namna familia zinavyowawekea hofu ya kushindwa kuolewa watoto wao wanapoonekana kuwa na elimu kubwa.



Balozi Liberata Mulamula akiapishwa na Spika Job Ndugai kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH WETU

# Wanafunzi Kaskazini wafagilia kuwezeshwa

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI katika shule za sekondari imani yao kubwa katika kufaulu na kuhudhuria madarasa kwa furaha ni namna ambavyo mwalimu anatoa ujuzi wake kwa kujiamini, mpangilio wa darasa lakini zaidi ni mazingira na vifaa vya kufundishia.

Kwa kuliona hilo, Benki ya NMB kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii wametenga kiasi cha asilimia moja ya faida ili kusaidia mambo mbalimbali ikiwamo elimu, afya na majanga mengine ya asili mara yatokeapo.

Miongoni mwa shule walizosaidia ni Shule ya Sekondari Kibacha na Shule ya Sekondari Kwakoko zilizopo mkoani Kilimanjaro, Wilaya ya Same, ambapo wanafunzi wanasema fadhila pekee wanayoweza kuwalipa NMB pamoja na wazazi wao ni kusoma kwa bidii.

Benki hiyo imesaidia viti 50 na meza zake katika Shule ya Sekondari Kwakoko ambapo pia wamesaidia viti 50 na meza zake katika Shule ya Sekondari Kibacha pamoja na vifaa vya maabara za sayansi za kujifunzia wanafunzi.

Wakizungumza na mwandishi wetu kwa nyakato tofauti, walisema wanajiona wana bahati kuwa sehemu ya utaratibu huo wa NMB kwa kuwa awali walisoma katika mazingira magumu lakini hawakuwa na namna ya kufanya.

Nasra Selemani wa Kidato cha nne Shule ya Sekondari Kibacha, alisema: "Tulikuwa wanyonge sana wakati tukikaa chini, hasa sisi wasichana kwa kuwa tulichafuka. Hatukuwa na utulivu wakati wa masomo kwa sababu wakati mwingine tulikaa wawili kiti kimoja. Lakini tangu tupokee msaada huu wa viti na meza kutoka NMB hata ufaulu umeongezeka na wanafunzi hawategei masomo."

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kibacha, Omary Magongo alisema, vifaa vya maabara za sayansi vimekuwa na tija kubwa kwao awali, lakini baadaye walipata changamoto ambayo wakisaidiwa maabara zitarejea katika kutoa mafunzo.

"Naweza kusema tumefaidika kwa kiasi kikubwa na NMB, siwezi kuelezea furaha yangu kwa maneno matupu. Hapa tuna wanafunzi kati ya 700 hadi 800, utaona ni idadi kubwa. Changamoto ya madawati ilitutoa jasho lakini nyinyi mmetusitiri.

Ofisa Uwajibikaji kwa Jamii kutoka NMB, Aloyce Kikois, alisema wengi wanadhani msaada huo unapatikana kwa kuandika barua ndefu au inayohitaji utaalamu mkubwa, lakini yeyote anaweza kuandika.

"Si lazima Mbunge au Mkuu wa Wilaya aandike barua ya maombi, hata mwanafunzi akiona shuleni kwake kuna tatizo la madawati, viti au vifaa vya kuezeka; aandike barua aipeleke kwa Meneja wa Tawi letu lililopo karibu naye, aainishe mahitaji na jina la shule asilikosee pamoja na wilaya na mkoa ilipo shule.

## Mfumo usafirishaji kwa mtandao rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya usafirishaji nchini (Bolt), imezindua mfumo maalum wa usafirishaji kwa njia ya mtandao inayojulikana kama Web App.

Meneja wa kampuni hiyo, Remmy Eseka, alisema lengo la kuzinduza huduma hiyo ni kurahisisha na kupunguza gharama zisizo za lazima.

Alisema mfumo huo mpya wa Bolt Web App, utatumiwa katika kuagiza usafiri wa aina mbalimbali kuhakikisha kuwa unapatikana kwa urahisi katika maeneo ya mjini.

"Kupitia Bolt Web App, wateja watakuwa na fursa ya kutoa taarifa kuhusu ubora wa safari yao na dereva husika na pia kupata fursa ya kupata usafiri wanaohitaji ikiwamo Bolt Boda, Bolt Bajaji na Bolt XL, ambapo mteja anaruhusiwa kuchagua aina ya usafiri anaotaka," alisema Remmy.

"Bolt Web App ni suluhisho sahihi kwa wanaomiliki simu za kawaida ambazo uwezo wake ni mdogo wa kimatumizi hususani katika kuhifadhi taarifa na wa kuunganishwa na huduma za mtandao. Mara nyingi watumiaji wa simu za aina hii pia wanajali gharama za matumizi ya data," alisema Eseka.

Alisema kupitia njia hiyo, watumiaji watakuwa na mbinu mbadala ya kuagiza usafiri kwa uhakika.

"Bolt Web App sasa tayari iko kwa watumiaji wa Dar es Salaam, Arusha na Mwanza pamoja na nchi za Afrika ya Kusini, Nigeria, Ghana na Kenya na Bolt ni mfumo wa usafiri unaolenga kufanya usafiri maeneo ya mjini kuwa rahisi, kwa uhakika na kwa gharama nafuu."

## Wanusurika ajali Mlima Kitonga

**Na Halfani Chusi**

WATU tisa wamejeruhiwa katika ajali ya basi la abiria aina ya Newforce, lenye namba za usajili T 715 DBK, iliyotokea katika Mlima Kitonga, mkoani Iringa, Wilaya ya Kilolo, Tarafa ya Mazombe, baada ya kugonga gema na kupoteza mwelekeo.

Basi hilo ambalo linafanya safari zake kutoka Dar es Saalam kwenda Mbeya, juzi 6:30, mchana liligonga gema lililokuwa pembezoni ya barabara na kupinduka papo hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva kushindwa kumudu gari lake.

"Ajali hii imetokea juzi hili basi lilikuwa limepakia abiria 52 wakati linateremsha mlima Kitonga mwishoni kabisa wakati linakaribia kumaliza mteremko liligonga gema na kupinduka papo hapo," alisema.




Ukurasa 13

Jamani 'media' zianze maisha upya



Ukurasa 12

SMZ ya Dk. Mwinyi, biashara ya jongoo 'mpango mzima' kilo sokoni Sh. 200,000/-




Ukurasa 14

**Wanavijiji wanogewa msaada mashine za magogo vijijini, sasa wadai nyongeza**

BUFE

IJUMAA APRIL 2, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

YANAYOJIRI CABO DELGADO...

# Ugaidi wageuza utajiri wa visima gesi laana ya mauaji Msumbiji?

**Na Moshi Lusonzo**

WAKATI nchi nyingi utajiri wa rasilimali ni kitovu cha neema kwa uchumi na maendeleo ya nchi, kwa Msumbiji ni sura inayokaribisha majanga kwao.

Hadi sasa kuna maharamia, wanamgambo wa Dola la Kiislam au 'IS' wanavyojulikana, wanazidi kujiimarisha na kuteka maeneo Kaskazini mwa Jimbo la Cabo Delgado. Nchini Msumbiji, ambako kuna historia ya kutotoa uhuru wa nchi hiyo wastani wa miongo minne na nusu iliyopita.

Kuongezeka nguvu kwa kundi hilo kumezidisha hofu ya usalama na kiuchumi kwa serikali ya nchi hiyo na mataifa ya nje.

Iko wazi wanamgambo hao wameshambulia na kuteka vijiji mbalimbali katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Tukio la hivi karibuni, ndilo limeishtua zaidi dunia, baada ya magadi wa IS walivyofanikiwa kuuteka mji wa Palma ambao ni kitovu cha utajiri wa gesi.



Wanakijiji wa Cabo Delgado, Msumbilji, wakiwa katika maisha ya simanzi, baada ya kuvamiwa. **PICHA: MTANDAO**

Ni uvamizi ambao raia wengi wameshafariki, wakiwamo wafanyakazi wa kampuni ya mafuta kutoka Ufaransa, ambayo ilitangaza kuanza rasmi kazi ya uzalishaji wa gesi katika visima vilivyopo ndani ya bahari, jirani na mji huo.

Pia kampuni zingine zenye vitalu vya uchimbaji gesi, zimesitisha kuwekeza mabilioni ya fedha katika maeneo ya pwani ya Cabo Delgado, kwa sababu ya kukosekana kwa hali ya usalama.

Wachambuzi wa uchumi wanaamini suluhu ya mgogoro unaoendelea utapatikana kupitia utawala imara na uwazi katika masuala ya uchumi, usawa katika umiliki ardhi, ajira na mgawanyo sawa wa mapato ya gesi.

"Pamoja na uasi tunaoshuhudia kuona, kampuni za kimataifa zinataka kujua kama wanaweza kuchukua hisa zao, lakini wanapaswa kuwaangalia wakazi wa eneo hili," anasema askofu mmoja wa Pemba.

### ANAWABEBA 'IS'?

Mkuu wa Operesheni Maalum wa Marekani barani Afrika, Meja Jenerali Dagvin Anderson, anasema kuwa kundi hilo limekuwa likipata msaada kutoka nje, hali inayolifanya kundi hilo kuwa hatari zaidi.

"Tumewashuhudia katika kipindi cha miezi 12 mpaka 18 wakijiimarisha uwezo wao wa mashambulizi na kutumia mbinu ambazo hutumika pia katika maeneo ya Mashariki ya Kati ambako kuna makundi yenye uhusiano na Islamic State," anasema Meja Jenerali Anderson.

Imani ya kuwapo watu nyuma ya kundi hilo, ni baada ya kuanza kumiliki magari ya kivita, silaha na sare za kisasa na Kaskazini mwa Msumbiji, sasa iko wazi zaidi kwa mujibu wa picha za video zilizopigwa katika eneo la Bandari ya Mocimboa da Praia, lililodhibitiwa.

Siku tisa, zilizopita wanamgambo hao walivamia na kudhibiti kwa siku mbili wanamgambo hao walidhibiti mji mwingine muhimu wa Quissanga.

"Sasa wana silaha na magari yanayowafanya waweze kutembea kirahisi na kufanya mashambulizi kwenye eneo kubwa na hutumia sare za wanajeshi. Hivyo, watu huchanganyikiwa na kuogopa," anasema.

Askofu wa Katoliki wa eneo la Pemba, Luiz Fernando Lisboa, anasema vitendo vya kigaidi dhidi ya wanavijiji vimesababisha watu 200,000 kukimbia makazi yao, huku shughuli za uzalishaji mali zikiwamo za kilimo na biashara zimesimama.

### KWANINI UVAMIZI?

Video tofauti zilizosambaa mwaka huu kwenye mtandao wa WhatsApp nchini Msumbiji, zinaonyesha kiongozi wa wanamgambo alitoa ufafanuzi kwa nini wanavamia na kuteka maeneo ya kimkakati.

Kiongozi huyo anadai wanafanya hayo kutokana na serikali kukosa usawa kwa watu wake, kuwadhalilisha maskini na kuwapa faida viongozi.

"Tatizo ni kuwa kuna kundi la vijana wasio na ajira. Ikiwa tutatatua matumizi ya nguvu, rushwa, na ikiwa tutakuwa na mfumo thabiti wa haki nina uhakika tutatatua shida hii haraka," anaeleza, mchambuzi Profesa Adam.

Hapo awali serikali ya Msumbiji ilitaka kupunguza uasi huo kwa kuwaita wanamgambo kama watu wahalifu, ilizuia waandishi wa habari kuingia katika mkoa huo. Hali ilivyo, sasa imebadilika serikali ya Msumbiji askari wa nje kutoka Urusi, Marekani na Afrika Kusini ili kusaidia jeshi kumaliza uasi huo.

***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa mtandao***

UCHUMI WA BULUU

# SMZ ya Dk. Mwinyi, biashara ya jongoo 'mpango mzima' kilo sokoni Sh. 200,000

• Aanzisha wizara maalum kuishughulikia • Yafungulia ajira maelfu vijana Zanzibar

**Na Christina Mwakangale**



Pierre Philippe Blanc, Mshauri wa Mradi wa Ufugaji wa Jongoo Bahari, uliosimamiwa na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), alipokuwa na wavuvi baharini. **PICHA MTANDAO**

ZANZIBAR ni sehemu ya Tanzania inayoundwa na visiwa vya Unguja na Pemba, kisiwa kilicho na umaarufu wa barabara zenye kona nyingi, milango iliyo na michoro tangu zama karne ya 19.

Mbali na kuwa Zanzibar ni kituo cha kihistoria cha biashara na uchumi wake kuimarishwa na utalii, hivi sasa uchumi utokanao na baharini unashika kasi, wakiwamo vijana 300,000 waliojiajiri tayari wanatarajiwa kunufaika.

Waziri wa wizara mpya ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi wa Serikali ya Zanzibar, Abdallah Hussein Kombo, anasema fursa zilizopo katika mazao ya bahari zinajumuisha jongoo wa baharini, walioko mjini Unguja, sambamba na uboreshaji uvuvi, mafuta na gesi.

Kimsingi, jongoo bahari au maarufu kwa jina la 'Sea cucumber' ni moja ya viumbe hai waliopo baharini. Hao ni kati ya biashara kubwa duniani, huku kukiwapo miradi mikubwa kwa nchi za bara la Asia, jongoo ni chanzo cha mapato, ajira na fursa muhimu za kuhifadhi viumbe baharini.

Hadi sasa Zanzibar inatajwa kuwa ya pili ukanda wa Afrika, katika kuanzisha ufugaji viumbe bahari hao, wakiwamo jongoo, huku wenzetu walio visiwani bara la Afrika, Madagascar, miradi ya namna hiyo imeshapiga hatua kubwa na hasa shughuli za ufugaji wa jongoo.

Waziri Kombo ana ufafanuzi katika hilo, akisema: "Rais Dk. Hussein Mwinyi alianzisha wizara hii mpya na aliona umuhimu kama njia kuu ya kuimarisha uchumi wa Zanzibar, ambayo imezungukwa na bahari," anatamka, akiwa na ufafanuzi hali halisi ya Zanzibar kuzungukwa na bahari, ni fursa ya kuimarika kwa shughuli za uvuvi.

"Uchumi wa Buluu ni suala jipya katika nchi yetu, tafsiri yake ni uchumi endelevu unaotokana na matumizi sahihi ya rasilimali za bahari. Kama ilivyo katika Ilani ya chama (CCM) namba 187 ikielezea uchumi wa buluu na ambao unaweza kuajiri takribani vijana 300,000," anasema, huku kuongeza:

"Uchumi wa Buluu Zanzibar, ni kwa sababu uchumi unaotokana na bahari ndio uchumi mkuu hasa kwa nchi za visiwa kama Zanzibar."

Anasema mkakati wa serikali ya Zanzibar katika uanzishwaji wizara unabeba maana ya kushughulikia uchumi huo, ikiwamo kutoa mafunzo kwa vijana, pamoja na uandaaji sera ambayo itatumika katika sekta hiyo.

> **"Uchumi wa Buluu Zanzibar, ni kwa sababu uchumi unaotokana na bahari ndio uchumi mkuu hasa kwa nchi za visiwa kama Zanzibar.**

"Tumejipanga kwanza kuweka mikakati ya watu wote waelewe kuhusu uchumi wa buluu kwa kushirikiana na sekta binafsi na nje ya nchi kuja kushirikiana na sisi katika uvuvi, mafuta na gesi kuja kushirikiana nasi," anasema Waziri Kombo.

Pia anataja kipaumbele katika sekta hiyo ni kwamba vijana watakuwa kati ya wanufaika wa uchumi huo na atahakikisha wizara yake itafika maeneo tofauti, ikiwamo vikundi na hata kuzungumza nao kuhusu sekta hiyo.

### MZIZI UFUGAJI JONGOO

Waziri Kombo anasema, biashara ya majongoo iliyoanzia miaka mingi iliyopita katika Bara la Asia, kwa upande wa Zanzibar ilianza kuibukia katika miaka ya 1990.

"Miaka hiyo biashara hii ilikuwa inafanyika tu baharini, lakini kutokana na kuongezeka



kwa kasi wa uvunaji na soko la bidhaa hii (jongoo) hasa kwa nchi za Mashariki ya mbali, pamoja na China, mashirika ya kimataifa na uhifadhi duniani, yalianzisha mfumo wa kufuga majongoo badala ya kuvuna tu baharini," anasema Kombo.

Anasema, 2015 ni mwaka ambao ushirika wa wakulima Hai ulianzisha uhamasishaji wa ufugaji majongoo kupitia vyombo vya habari, kwa kujenga mashamba ya viumbe hao na hata wakaonyesha matokeo chanya.

Kombo anasema, ndiko ufugaji ulipoanza kuonekana chanya na SMZ iliamua kupeleka wataalamu 30 nchini China, ambao sasa wamebobea katika ufugaji wa mazao ya baharini, ili kuendeleza sekta hiyo.

Pia waziri huyo anabainisha kwamba, ilpofika mwaka 2012, idadi kama hiyo ya wataalamu walisafiri kwenda kujifunza mwaka 2017, wataalamu kutoka China wakifika visiwani humo kutoa mafunzo ya mwezi mmoja kwa wataalamu 30 wa Zanzibar.

Kwa mujibu wa Waziri Kombo, watumishi wa sekta hiyo, pia walipata fursa ya kuhudhuria mafunzo yahusuyo ufugaji baharini nchini China.



Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Zanzibar, Abdallah Hussein Kombo.

Anasema mwaka 2019 kupitia mpango wa uendelezaji sekta ya ufugaji na mazao ya baharini wataalamu wa Madagascar, walifika visiwani humo kupitia Taasisi ya Blue Venture, waliotoa mafunzo ya ufugaji bora majongoo na ujenzi wa maeneo ya kufugia.

### WAFUGAJI WAIBUKA

Umuhimu wa ufugaji huo, ulipobainika, anasema sasa kipaumbele kinatolewa katika ufugaji jongoo na biashara inaimarika, ikiwamo kukuza uchumi.

"Mimi na Mwinyi ni miongoni mwa taasisi za kijamii ambazo zina azma ya kutekeleza malengo hayo. Wizara itatoa ushirikiano kwa taasisi kama hizi zote, ili kboresha ufugaji," anasema.

Waziri anaongeza: "Nitoe wito kufuata kanuni na sheria za uvuvi, ili kutunza mazingira."

Msisitizo wake sasa ni kwamba, bahari ndio uchumi mkuu na tegemezi wa visiwa vya Zanzibar, kutokana na mazingira yake kuzungukwa na bahari na kwamba lengo la wizara hiyo mpya ni kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Kutokana na hilo, waziri huyo, anatoa wito kwa vijana visiwani humo, kujiajiri katika biashara itokanayo na mazao ya bahari, hususan uvuvi wa samaki na majongoo, mwani, chumvi, mafuta na gesi na kubadili hali zao kimaisha.

### WADAU WAKE

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mimi na Mwinyi, Salmin Shukuru Botea, anasema wamelenga kukuza fursa za mwamko wa vijana kutaka kujifunza katika shughuli hiyo hasa ufugaji wa majongoo ni mkubwa, ingawa changamoto ni kuwafikia.

"Uchumi upo katika bahari, niwaambie tu hivyo vijana. Kilo moja ya majongoo huuzwa hadi shilingi laki mbili, ukiwa na kilo 40 una shilingi milioni 80 wa mwaka. Vijana tuna akili na nguvu tunangoja nini?" Anasema

"Ni wakati wa kufuga jongoo, samaki ambao hauhitaji gharama kama ambavyo utafuta kuku," anaendelea Salmin, akiwa na misisitizo: "Hii ni fursa kwa vijana kujiajiri katika shughuli ya uvuvi wa majongoo na ufugaji ili kujiongezea kipato. Nilipoanzisha taasisi hii, lengo lilikuwa kukuza ajira, biashara na uchumi."

Anasema, matarajio yao ni kuanzisha ufugaji na uvunaji wa jongoo kirahisi na usiohitaji uwekezaji mkubwa kama ilivyo uvuvi wa samaki, unaohitaji nyavu na boti kupata kupata mazao zaidi.

Katibu wa Ushirika wa Wakulima Hai Co-operative Society, Zanzibar, Semeni Mohamed Salum, anasema biashara ya jongoo, ilianza visiwani mwaka 2011 na kwamba ufugaji ulikuwa vijijini zaidi.

"Ufugaji huu una tija! Serikali imeahidi sekta hii itaipa nguvu ufugaji baharini kwa kuwa mwamko ni mkubwa, waliojiajiri katika uchumi wa buluu, soko lipo kubwa, ikiwamo hasa Hongkong na Marekani," anasema Semeni.

### MTAALAMU JONGOO

Pierre Philippe Blanc, ni mtaalamu na Mshauri Mkuu wa Mradi aliyebobea katika uzalishaji jongoo, kutoka Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) la Umoja wa Mataifa, anasema jongoo ni bidhaa anayeweza kuleta mageuzi makubwa Zanzibar na ukanda wote wa Afrika,

Akizungumzia mwaka juzi katika mazungumzo ya kimataifa mwaka juzi, anasema Zanzibar wana uwezo wa kuzalisha hadi ziada majongoo wadogo na kusambaza mbali kwa ukanda wananchi kama Madagascar na maeneo mengine ya ukanda wa Bahari ya Hindi.

Mradi unaoendelea sasa Zanzibar, ulianza kwa ufadhili wa asasi ya KOICA kuoka nchini Korea Kusini, huku FAO, wakihusika na masuala ya utaalamu.


Mtaalamu huyo Pierre, kutoka FAO, anasema huenda ukawa mzizi wa mageuzi makubwa katika uchumi wa Zanzibar, kutokana na kuwapo soko kubwa la jongoo katika nchi za bara la Asia na Ulaya.

Utafiti wa awali wa Shirika la Misaada la Korea (KOICA), uliofanywa mwaka 2012 na ulipendekeza kuendelezwa kwa sekta ya uvuvi kutokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya vyakula vya mazao ya baharini, hali ambayo inaweza kusababisha baadhi ya viumbe hai bahari kutoweka.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Jamani 'media' zianze maisha upya






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

UNATOKEA kuwa miongoni mwa watu wanaoishi katika mazingira ya baridi kali. Unajua kwamba ni ngumu kwa binadamu kuishi katika hali kama hiyo, hivyo unahakikisha kuwa unanunua masweta kwa ajili ya familia yako.

Na kwa kuwa unajua fika kwamba baridi inaumiza na wewe unaitumia kama adhabu kwa wanao wanaokukosea au kukiuka maadili ya familia, kwa kuwanyima sweta, ili wajutie makosa yao ili wasiyarudie.

Adhabu hiyo unaitoa kwa vipindi tofauti, kutegemea uzito wa makosa, wengine wanaweza kukaa bila sweta kwa wiki, mwezi hata miezi na hasa wale ambao ni kiburi wasiotaka kujirudi angalau hata kwa kuomba radhi.

Lakini, wakati adhabu zako zikiendelea, baadhi ya majirani zako wanaingiwa huruma na kuwaombea msamaha, na hata wengine kuwatupia mashuka au vitenge na hata khanga, angalau kuwapunguzia mateso ya baridi.

Hatimaye, baadhi ya walioombewa msamaha unawapa sweta na wanaendelea na maisha yao kama kawaida, huku wengine pengine bado wanaendelee na adhabu.

Hivi karibuni, kituo kimoja cha redio na televisheni, kilipunguziwa adhabu kutoka miezi sita hadi takriban mmoja kutokana na kosa la maadili.

Baada ya kuomba radhi huku pia, watu wengine wakishiriki kuwaombea radhi, mlezi ambaye ni serikali akaamua kuwapunguzia adhabu iliyokuwa imelenga televisheni na sasa wanaendelea na matangazo yao kama kawaida.

Pongezi kwa serikali, kwa kuonyesha ulezi mwema kwa watoto wake. Kuna baadhi ya vyombo vya habari vilivyofungiwa na serikali baada ya kuonekana kuwa na hatia ya kukiuka maadili ya utangazaji na utoaji habari, vingine vilikata rufani katika mamlaka zilizoko na kushinda, bado havijarejea kazini kutokana na sababu mbalimbali.

Vyombo hivyo vilikuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha jamii, pia ya kuwa pia vyanzo vya mapato kwa wamiliki, pia watumishi, ambao nao wana familia zinazowategemea.

Kwa maana hiyo, baridi ya kufungiwa inawapiga wamiliki, watumishi na familia zao, kiasi kwamba ni huruma tu ya mlezi, ndiyo inayosubiriwa katika ama kuvipunguzia adhabu kwa kuvifunika kwa mashuka, au kuvifutia kabisa adhabu kwa kuvirejeshea sweta.

Magazeti na vituo vya redio na televisheni vilivyofungiwa, kwa kweli kutokana na muda ulivyokwishapita, vina kila sababu ya kuwa vimejitambua na kujirudi na kuona umuhimu wa kuzingatia maadili na kuendelea na majukumu yao ya msingi, endapo tu mlezi ataona umuhimu huo.

Nadhani inawezekana, mathalani kwa waziri au mawaziri wenye dhamana kwa niaba ya mlezi, serikali, kutoka hadharani na kutangaza msamaha wa jumla kwa vyombo vilivyo kifungoni, kama afanyavyo Rais kusamehe maelfu ya wafungwa ufikapo wakati mwafaka wa kufanya hivyo.

Narejea kuipongeza serikali kwa hatua iliyochukua kuisamehe, lakini kuitaka huruma iwafikie na wengine waliofungiwa wafunguliwe, ili kuokoa maisha ya wamiliki, wafanyakazi na wategemezi wao.

Si rahisi kwa mwana kumlazimisha mzazi amsamehe, bali ni rahisi kuomba kusamehewa kwa kujutia makosa yaliyofanyika na mzazi anayejua umuhimu wa kutokata mkono ulionajisiwa na mwana, husamehe na kuanza upya, ili maisha yaendelee kwa maslahi mapana ya jamii. Alamsiki!

UCHUMI

# Wanavijiji wanogewa msaada mashine za magogo vijijini, sasa wadai nyongeza

## • Ni wanufaika mradi wa FORVAC

**Na Christina Haule**, RUANGWA




Mkurugenzi wa Shirika la Kuendeleza Uhifadhi wa Mpingo (MCDI), Jasper Makala, akimweleza Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (mwenye miwani nyeusi) na viongozi wa kiserikali mkoani Lindi, jinsi mashine ya kuchakata magogo inavyofanya kazi, baada ya waziri kuzindua. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

WANAVIJIJI kutoka vijiji 18 vya wilaya za Ruangwa na Nachingwea mkoani Lindi, wako katika tabasamu ya kupatiwa nyenzo ya kiuchumi, mashine ya kisasa ya kuchakata magogo.

Ila wana lao lingine la kuiomba serikali, kwa kushirikiana na Mradi wa Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC), ihakikishe kila wilaya inakuwa na mashine yake ya kuchakata magogo, hali itakayowasaidia kukua kiuchumi kwa wakati.

Hizo ni kauli zao baada ya kupokea mashine ya kuchakata magogo maarufu 'Mobile Somi' yenye thamani ya Sh. milioni 110, iliyotolewa na serikali ya Finland, kwa kushirikiana na serikali kupitia mradi wa FORVAC.

Mbali na shukurani wanayoitanguliza, wanatamka kwa nyakati tofauti kwamba, mashine hiyo moja iliyotolewa itumiwe na wilaya hizo mbili, bado ni kikwazo katika ufanisi wa utendaji kazi wao.

Mkazi wa kijijini Mbondo, wilayani Nachingwea mkoani Lindi, Haji Mwembe, anaishukuru serikali kuwapatia mashine hiyo anayoamini itawainua katika uchakakati mbao na kupata mauzo makubwa, tofauti na mwanzo.

Anasema, kuna haja ya serikali kupitia FORVAC, ikawapatia mashine nyingine kwa kila wilaya, hali anayoamini kwa kuhudumia wilaya mbili za Nachingwea na Ruangwa, haikidhi vyema mahitaji inavyostahili.

"Mashine ya kuchakata mbao zinapaswa ziwe kila wilaya na ya kwake, tukitumia moja sote bado italeta shida, tunaomba FORVAC mtuletee mashine yetu, tuweze kuchakata wenyewe bila kufuata zamu au kusubiri kupokezana," anasema.

Mratibu wa Kitaifa wa Programu ya Mnyororo wa FORVAC, Emmanuel Msoffe, anasema FORVAC itahakikisha kila wilaya inapata mashine yake kulingana na kongani tatu za mradi zilizopo.

Msoffe, ambaye ni Ofisa Misitu na Nyuki Mwandamizi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, anasema kuna mpango wa kununua mashine zingine nne wanazotarajia hivi karibuni, watazigawa kwenye kongani zilizopo kitaifa.

Anazitaja kongani za miradi hiyo ni mkoani Tanga katika wilaya za Handeni, Kilindi, Kiteto na Mpwapwa; Ruvuma, wilayani Tunduru, Namtumbo, Songea, Mbinga na Nyasa; na mkoani Lindi katika wilaya za Nachingwea, Ruangwa na Liwale.

Msoffe anasema tayari kuna mashine mbili zimeshagawiwa, moja wilayani Songea, Nachingwea na Ruangwa.

Anafafanua kuwa, ugawaji mashine hizo utazingatia mita za ujazo wa miti iliyopo katika wilaya husika, kwa wananchi walioandaa uvunaji miti yenye ujazo wa kuanzia mita 100.

Msoffe anasema, katika kuhakikisha mashine zinafanya kazi vizuri, watawakusanya wanaoziendesha kupatia mafunzo, ili kuwapo ufanisi kulingana na malengo yanayokusudiwa.

### FAIDA ZILIZOPATIKANA

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, anawataka wakazi kutodharau mashine walizokabidhiwa kutokana na udogo iliyo nao, bali waangalie faida zake anazozitaja kuwa kubwa.

Anasema, walipatiwa mashine kutoka Shirika la WWF mwaka 2017, iliyowasaidia kimaendeleo kati ya vijiji 11 vyenye mradi wilayani na tayari vijiji vitatu vimeshaanza kuchakata magogo kwa kutumia mashine, huku wakioona faida zake.

Ngubiagai anasema kijiji cha Mkea, kimeshapata Sh. milioni 34 baada ya uchakataji magogo, tofauti na uchakataji wa zamani kienyeji, kabla ya hiyo zilipoteza ujazo mkubwa wa mbao na ilikusanya Sh. milioni 26, ambayo Sh. milioni sita pungufu ya pato la sasa.

Anasema, kijijini Libwichi walikotumia teknolojia ya zamani, walipasua mbao za mita za ujazo 154 na kupata Sh. milioni 25, lakini walipotumia mashine za kisasa kwa mbao za ujazo huo huo, walipata jumla ya Sh. milioni 67.

Mkuu wa Wilaya anakitaja kijiji kingine cha Likawage, anayesema teknolojia za zamani iliwaingiza cha Sh. milioni 45, kutoka jumla ya mbao zenye mita za ujazo 167.

Anasema kinyume chake, walipochakata mbao kwa kutumia mashine za kisasa, waliingiza jumla ya Sh. milioni 141.4.

Ngubiagai anaongeza kwamba mashine hiyo yenye teknolojia rahisi wilayani Kilwa, imewafunza mengi katika mapato endelevu ya misitu, yanayowawezesha kumalizia ujenzi wa madarasa yaliyokuwa hayajakamilika katika shule zao za msingi na sekondari.

Mengine anayotaja ya kunufaika, inajumuisha ujenzi wa zahanati, nyumba za walimu, madawati, kuwakatia bima za CHF wanavijiji, kupatikana sare za wanafunzi na chakula cha wanafunzi shuleni.

### WAZIRI DK. NDUMBARO

Waziri wa Maliasili na Utalii Dk. Damas Ndumbaro, anaishauri FORVAC, kutafuta namna ya kuongeza mashine hizo, ili kuwezesha teknolojia rahisi kwa wananchi, aliyoieleza ni njia sahihi ya kuzalisha maendeleo vijijini.

Dk. Ndumbaro anasema, ni mashine zitakazosaidia kuchakata magogo kupitia utaratibu wa kisheria, unaoenda na vijiji kutanuka kimaendeleo katika sekta mbalimbali zikiwamo elimu, afya na miundombinu.

Aidha, anasema ni sehemu ya mkakati na mipango ya kitaifa inayowataka wanavijiji kuongeza mapato na maendeleo, wakitumia mashine hiyo rahisi na mahususi kwa kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao misitu.

Waziri Dk. Ndumbaro, anasema mashine za sasa zinawapatia wanavijiji asilimia 60 ya mapato tofauti na zamani, zilizowapatia asilimia 30 pekee.

"Pia mashine hii inapunguza upotevu wa mazao ya misitu na kutengeneza ajira kwa wananchi na itazalisha ajira zaidi 250. mashine ni rafiki kwa mazingira, inatumia miti michache kwa manufaa makubwa, " anasisitiza Dk. Ndumbaro.

Waziri huyo anawataka viongozi wa halmashauri za wilaya kuwa macho kusimamia sheria kudhibiti uvunaji misitu kiholela, ikiwamo kuchukua hatua dhidi ya wakiukaji wote.

Dk. Ndumbaro anawakumbusha wananchi, kwamba vibali vya uvunaji misitu vinatolewa na vijiji pekee na mhitaji wa kununua mbao, sharti akatiwe na wanavijiji kupitia vikundi vyao rasmi, jambo linalorahisisha ukusanyaji kodi vijijini.

Pia waziri anasema ukusanyaji mzuri wa kodi za mazao hayo ya misitu kupitia FORVAC, unasaidia kuanzishwa na kuboreshwa miradi ya vijiji, anawaagiza wakuu wa wilaya zenye miradi ya uvunaji endelevu wa misitu, kusimamia, tija yake kwa manufaa ya wanavijiji.

Lingine anawaagiza wadau wa misitu, katika wilaya na halmashauri kuhakikisha wanasimamia uhifadhi wake, kwa kuzingatia uvunaji unaoendana na uhifadhi, ili kutopoteza misitu iliyopo.

### MKURUGENZI MISITU

Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, anaainisha kwamba, vijiji vitakavyonufaika na mashine hiyo, vimeshaandaa mipango endelevu ya kusimamia misitu wakisaidiwa kitaalamu na mamlaka hiyo ya kiserikali.

Anasisitiza haja ya matumizi yote ya misitu kuzingatia mipango ya usimamizi, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na FORVAC.

"Kamati za maliasili za vijiji zimepewa mafunzo stahiki kuwawezesha kutekeleza vyema majukumu ya usimamizi shirikishi wa misitu, kwa niaba ya wananchi.

"Hivyo mashine uliyozindua leo na nyingine kati ya mbili utakazozindua hivi karibuni, ni sehemu tu ndogo ya utekelezaji wa mradi wetu mkubwa wa FORVAC," anasema Dk. Mwakalukwa.



# Ndalichako atoa mwezi mmoja kupata taarifa ukaguzi shule

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, amemwagiza Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti Ubora nchini kumpelekea taarifa ya ukaguzi wa shule na walichokibaini katika ukaguzi huo ndani ya mwezi mmoja.

Akizungumza juzi katika hafla ya kukabidhi magari 38, kwa wadhibiti ubora wa shule Prof. Ndalichako alisema, anatoa mwezi mmoja kwa mkurugenzi huyo kumpelekea ripoti ya tathmini ya shule hizo.

Alisema haridhishwi na mfumo wa ukaguzi unaotumika sasa ambao alisema unasababisha kufanya matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma.

"Tunagawa magari haya kwa ajili ya wadhibiti ubora wa shule kuwawezesha kuzifikia shule kwa wingi na kwa wakati, lakini cha kushangaza mdhibiti ubora ataendesha gari kutumia mafuta ya serikali kwenda kata ambako kuna shule ya msingi na sekondari, lakini atakagua shule ya msingi na kuiacha sekondari.

"Halafu nataka mwingine aje kukagua sekondari, hayo ni matumizi mabaya ya fedha za umma, nilishatoa maelekezo wadhibiti ubora msingi wawe na uwezo wa kukagua na shule za sekondari, haiwezekani magari mawili yapishane kwenye kata hiyo hiyo kufanya ukaguzi," alisema. Alisema, hali hiyo pia inasababisha shule zinazofikiwa kuwa chache.

"Mkurugenzi nenda na wakati mimi nataka mkurugenzi anayeenda na wakati kama huwezi tutafuta wadhibiti ubora wa shule wanaokwenda na wakati ili tuwe na matumizi mazuri ya rasilimali, na kama Mkurugenzi huwezi kwenda na wakati katibu mkuu nakuagiza kutafuta mkurugenzi mwingine," alisisitiza.

Prof. Ndalichako alisema, serikali inaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo pamoja na wadau mbalimbali katika kuboresha elimu nchini.

Aliwashukuru wahisani na wadau wa maendeleo wakiwamo Benki ya Dunia, SIDA pamoja na DfID ambao kupitia mradi wa Lipa kwa Matokeo (EP4R) wamewezesha ununuzi wa magari 38, kwa gharama ya shilingi bilioni sita.

Alisema lengo la magari hayo ni kuimarisha shughuli za udhibiti ubora wa shule nchini.

"Magari haya yanagawiwa kwenye halmashauri 27, zisizo na magari, kanda 10 na gari moja litatumika katika ofisi ya makao makuu ya wizara kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji.

Alisema, wizara yake kupitia idara ya udhibiti ubora wa shule ina jukumu la kusimamia mfumo wa udhibiti ubora wa shule na kufanya tathmini ya ujifunzaji na ufundishaji katika shule na vyuo vya ualimu na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu, wakufunzi na viongozi wa elimu ili kuinua ubora wa elimu nchini. Vilevile alisema, serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa udhibiti ubora wa shule kwa kuongeza wadhibiti Ubora wa shule wapya 400 katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 ongezeko ambalo limesaidia kuleta tija katika ufuatiliaji shuleni katika vyuo vya ualimu.

Pia alisema katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi serikali imeshatumia kiasi cha Sh. bilioni 15.203 kwa ajili ya kujengwa ofisi 100 za wadhibiti ubora wa shule katika halmashauri za wilaya na kwa sasa inaendelea na ujenzi wa ofisi 55 na ukarabati wa ofisi 31 kwa gharama ya Sh. bilioni 11.256.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, aliwataka wadhibiti ubora wa shule kuyatumia magari hayo kwa malengo yaliyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Moshi Kabengwe, alisema magari hayo yamepewa kwa wadhibiti ubora wa wilaya, kanda na halmashauri zenye upungufu wa magari na ambazo magari yake yamechakaa.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa ugawaji wa magari 38 kwa ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda na Wilaya nchini, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga (wa pili kulia), Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu, Moshi Kabengwe (wa pili kushoto), Mhasibu Mkuu Nicodemus Mallya (kushoto) na Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule, Euphrasia Buchuma. **PICHA: WIZARA YA ELIMU**

## Wafanyabiashara watakiwa kuongeza thamani bidhaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Tawala msaidizi sekta za uchumi Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, amewaagiza viongozi wa umoja wa wafanyabiashara wa soko la Sabasaba jijini Dodoma, kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuongeza thamani ya bidhaa zao.

Agizo hilo lilitolewa kwa wafanyabiashara wa soko hilo kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi uliofanyika juzi jijini hapa.

Mumba alisema kuwa nafasi walizokabidhiwa wahakikishe wanawajibika kuhakikisha wanaboresha mazingira ya soko ili wafanyabiashara waweze kufanya shughuli zao kwa uhuru na uwazi bila kuvunja sheria na taratibu zilizowekwa na jiji.

"Baada ya zoezi hili ni matumaini yetu ofisi ya Mkuu wa Mkoa, jiji pamoja na wadau wanaotumia soko ni wajibu wenu nyinyi viongozi kuwa na jukumu la kuhakikisha mnaboresha soko lenu, pia ninawaomba mvunje makundi yote kwa wale waliokuwa wagombea ili mfanye kazi kwa umoja na mshikamano," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa soko hilo, Athumani Makole, alisema kuwa kwa miaka mitatu hawana uongozi na wafanyabiashara wanakosa fursa mbalimbali za kuwezeshwa mikopo.

Alisema kuwa kuchaguliwa kwao hivi sasa watahakikisha pia wanatekeleza maagizo kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ili soko hilo liwawezeshe wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika mazingira yaliyoboreshwa huku pia wakifuata kanuni, sheria na utaratibu kama zinazoelekeza na jiji.

Makamu Mwenyekiti wa soko hilo, Kombo Adamu Kombo, alisema watafanya kazi zao kwa malengo ya kuunga mkono serikali inayohimiza kila Mtanzania kufanya kazi kwa bidii. "Baada ya kukaa kwa muda mrefu bila kuwapo kwa uongozi ndani ya soko hili, tutahakikisha tunafanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja na serikali na kutimiza malengo yetu ili tuweze kujiinua mitaji ya biashara zetu kwa kila mfanyabiashara," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Viwandani, Emmanuel Nyenje, aliwataka wafanyabiashara hao kusahau yaliyopita ndani ya miaka mitatu, wafanye kazi ili wajiimarishe kiuchumi na kujiepusha na migogoro.

# Afanya ujasiriamali kwa fedha za TASAF

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

MNUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), Mwanjala Said, ameamua kufanya ujasiriamali kwa kutumia akiba alizowezeshwa kuanzisha biashara ya kukopesha sukari kwa wafanyabiashara wadogo, kijiji cha Goima.

Mwanjala, ambaye ni mnufaika wa TASAF yeye na familia yake alianza kufanya biashara hiyo akiwa na mtaji wa Sh. 120,000 ambazo alitumia kununua mfuko wa sukari.

Akizungumza katika ziara ya kutembelea wanufaika wa mpango huo, Mwanjala alisema biashara ya kuuza sukari kwa wakazi wa kijiji cha Goima alianza kupitia fedha za TASAF ambazo walipewa kwa ajili ya kujikimu na alipoweka akiba kidogo kwa muda wa miezi kadhaa na kufanikiwa kupata mtaji.

"Naishukuru sana serikali kupitia mpango wa TASAF kwa sababu umenisaidia kuanzisha biashara ambayo naitumia kujikimu mimi na familia yangu," alisema Mwanjala.

Alisema fedha inayotolewa akipangilia vizuri anaweza akatengeneza kitu kikubwa ambacho kitakuwa kikimwingizia faida itakayosaidia kuendesha maisha ya kila siku.

Pia amekuwa akifuga kuku na mbuzi wanaompatia fedha za kujikimu na familia yake ikiwamo kununua vifaa vya shule vya wanafunzi. Alisema bila mpango wa kunusuru kaya maskini asingeweza kupiga hatua moja mbele kimaendeleo kama alivyo sasa.

Kutokana na hilo amewashauri wakazi wa kijiji hicho na vijiji vingine wakipewa fedha waitumie kwa kufanya jambo ambalo litawasaidia kuwapa maendeleo.

Naye mlengwa Ashura Bela, alisema mpango wa kunusuru kaya maskini umewasaidia wakazi wa vijiji mbalimbali kujiinua kiuchumi kutokana na fedha ambayo wamekuwa wakipata na kuitumia katika biashara ndogo ndogo.

"Kwa kweli TASAF, imetuinua sana walengwa wa mpango huu kila tunapopewa fedha za kujikimu huweka akiba na kubuni biashara," alisema Bela.

Ofisa Malalamiko wa Idara ya Mawasiliano TASAF, Makwinja Yusuph, alisema TASAF imekuwa ikitoa mafunzo kwa walengwa wa mpango huo kupitia wataalamu mbalimbali kuwaelekeza namna ya kuibajeti fedha hiyo.

Alisema kuna wasimamizi ambao kama mlengwa anahitaji kufuga au kuendesha kilimo basi humpa mbinu za jinsi ya kuendesha ujasiriamali mdogo ambao anataka kufanya kupitia akiba ya fedha aliyojiwekea kutoka TASAF ikiwamo mitaji ambayo hutolewa kwa wasichana kwenye mradi wa timiza malengo.

Alisema walengwa wengi wa mpango wa kunusuru kaya maskini wamejikita kufanya biashara ndogo na ufugaji kutokana na akiba wanazojiwekea wanapopata ruzuku kutoka TASAF.



## Bonde Ziwa Rukwa kufanyiwa usafi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BONDE la maji la Ziwa Rukwa kwa kushirikiana na shule za msingi na sekondari 13 za jijini Mbeya, limeanzisha kampeni maalum ya kufanya usafi wa mazingira kuzunguka vyanzo vya maji ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji unaosababishwa na shughuli za binadamu.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chitanda, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe kihusiana na namna walivyojiandaa kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Alisema katika kukabiliana na tatizo la uharibifu wa vyanzo vya maji wameanzisha kampeni ya kufanya usafi kuzunguka vyanzo hivyo huku wakitoa elimu kwa jamii kuachana na tabia ya kuharibu mazingira.

"Kampeni yetu ya usafi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji tutaifanya kwenye bonde la mto nzovwe ambalo humwaga maji yake ziwa rukwa kwa sababu bonde hilo sasa limevamiwa na shughuli za binadamu ikiwemo utupaji wa taka na mizoga," alisema Chitanda.

Aliongeza kuwa tatizo la uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji hususani utupaji wa mifuko ya plastiki imechangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa viumbe hai katika mito na vyanzo vingine.

Mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Utengule, Valeria Angumbwike, aliomba serikali kuziwezesha shule kutengeneza vyama vya mazingira ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Alisema vyama hivyo vitajikita kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa kutunza mazingira katika vyanzo vya maji. Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyata, alisema kuwa asilimia 60 ya magonjwa ya binadamu yanatokana na matumizi ya maji yasiyo salama ambayo kwa kiasi kikubwa yanachotwa mtoni. Aliitaka jamii kuunga mkono jitihada za serikali katika kampeni ya usafi wa mazingira ili kuhamasisha utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

# Mafuriko yaleta athari kubwa Kyela

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WANANCHI wa kata za Mababu na Matema wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya, wamekumbwa na mafuriko baada ya daraja ambalo ni kiunganishi cha maeneo hayo kusombwa na maji pamoja na kuharibu miundombinu ya barabara.

Mafuriko hayo yamesomba mifugo 20 zikiwamo ng'ombe, mbuzi na nguruwe pamoja na kuharibu mazao mashambani.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Katumba Kata ya Mababu, Lwimiko Anyosisye, alisema kubomoka kwa daraja hilo kumeathiri shughuli za uzalishaji ikiwamo kilimo na biashara.

Alisema daraja hilo ni tegemezi kwa wakazi wa Katumba kwenda maeneo mengine kupata huduma muhimu za kijamii ikiwamo shule na vituo vya kutolea huduma.

"Zaidi ya mifugo 20 imesombwa na mafuriko, baadhi ya nyumba za watu zimesombwa, mazao shambani pia hali ni mbaya hasa kwa mvua iliyonyesha Machi 29, mwaka huu, ilileta madhara makubwa sana," alisema Anyosisye.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Katumba, Adamson Mwaikinda, alisema daraja hilo kila msimu linaharibika na kwamba tangu mwaka 2015 lijengwe limekuwa likibomoka na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa ili kuboresha miundombinu imara itakayoweza kuhimili mafuriko.

Alisema hadi sasa wanafunzi wameshindwa kwenda shuleni kutokana na mawasiliano ya daraja kubomoka pamoja na miundombinu ya barabara.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mababu, Yona Mwakalendile, alisema hofu kubwa ni kwa watoto kusombwa na mafuriko kwa sababu mvua zinazoendelea kunyesha ni kubwa.

Alisema hitaji lao kwa sasa ni kujengewa miundombinu imara ya daraja hilo tegemezi na kurekebisha barabara zilizoharibiwa na mafuriko ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji mali kama ilivyokuwa awali.

Diwani wa Mababu, Rashid Yahya, alisema tangu mwezi Machi mvua ziliendelea kunyesha lakini iliyonyesha Machi 30 ilikuwa kubwa sana na kusababisha madhara.

Alisema wananchi wanahitaji kujengewa miundombinu ya kudumu ili kutokwamishwa kufanya shughuli zao za kujikwamua kiuchumi ikiwamo kilimo, ufugaji na ujasiriamali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alitoa pole kwa wananchi waliopata adha kutokana na mafuriko na kuwahakikishia kuboreshwa kwa miundombinu yote iliyoathiriwa na mvua.

Alisema atakaa na wataalamu kujadiliana namna bora ya kuboresha miundombinu hiyo ikiwezekana kutenga bajeti maalum ili kukarabati na kujenga miundombinu ya barabara na daraja hilo tegemezi kwa uchumi wa Kata za Mababu na Matema.



Wananchi wa Kitongoji cha Katumba, Kata ya Mababu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya, wakiwa juu ya daraja kitongojini hapo jana, wakiangalia uharibifu uliofanywa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha katika daraja hilo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakulima wa ngano waomba bei elekezi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa zao la ngano, mkoani Mbeya, wameomba serikali kutoa bei elekezi ya zao hilo ili kuwanusuru na unyonyaji unaofanywa na walanguzi ambao wananunua mazao kwa bei ya chini ikilinganishwa na gharama za uzalishaji.

Wakizungumza kwenye mkutano wa uhamasishaji wa kilimo cha zao hilo ulioandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole (TARI), Mkoa wa Mbeya na kufanyika katika kijiji cha Usoha Kata ya Muungano wilayani Mbeya, walisema wamekuwa wakilazimishwa kuuza mazao yao kwa bei ya kati ya Sh. 8,000 na Sh. 15,000 kwa ndoo ya plastiki yenye ujazo wa lita 20.

Mmoja wa wakulima hao, Michael Mbugu, aliiomba serikali kutafuta mbinu za kuwasaidia wakulima wasidhulumiwe na walanguzi hao kwa kununua ngano kwa bei ya kutupa kwani wamekuwa wakitumia nguvu na gharama kubwa katika uzalishaji wa zao hilo na kwamba bei hiyo haiwanufaishi.

"Tunaomba serikali isikie kilio chetu kwamba tunatumia nguvu kubwa kuzalisha ngano, lakini kutokana na walanguzi kununua mazao yetu kwa bei ndogo hatuwezi kunufaika na mazao yetu hivyo tunaiomba serikali iingilie kati kwa kupanga bei elekezi ambayo itazingatia gharama za uzalishaji," alisema Mbungu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema kuwa ipo changamoto ya maofisa kilimo kutofika kwa wakulima kusikiliza kilio chao na kuagiza kuwa kuanzia sasa wafike katika kijiji hicho kuzungumza na wakulima na kutatua tatizo hilo.

"Mkoa wa Mbeya una ardhi yenye rutuba nzuri ya kilimo, lakini tatizo lipo kwa maofisa kilimo kutowatembelea wakulima na kuwashauri mbinu bora za kilimo ikiwa ni pamoja na namna ya kupunguza gharama za uzalishaji, hivyo kuanzia sasa nawaagiza maofisa ughani kuwatembelea wakulima kila walipo na kutatuan changamoto zao," alisema Ntinika.

Kuhusu changamoto ya bei ndogo ya zao la ngano, Ntinika aliwataka wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalamu ili wazalishe mazao yaliyo bora ambayo yatajiuza yenyewe kwa bei nzuri yakifika sokoni.

Mtafiti wa zao la ngano, Dk. Rose Mongi, alisema kuwa wamezalisha mbegu za kutosha na kwamba wanatarajia kuzigawa kwa wakulima zaidi ya 400 pamoja na kuwapatia elimu ya kitaalamu ya uzalishaji.

Alisema uzalishaji wa zao hilo bila kuzingatia elimu ya kitaalamu na matumizi ya mbegu bora ni sababu ya wakulima kupata mazao kidogo ambayo yanakandamiza uchumi wao.

Dk. Mongi alisema wameanzisha mradi wa kuwezesha wakulima katika kilimo cha ngano kwa ufadhiri wa Benki ya Afrika baada ya kubaini kuwa kilimo cha zao hilo kina tija katika kuwakwamua wananchi kiuchumi.





# Wananchi waomba kushirikishwa miradi ya maeneo yao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imeshauriwa inapoanzisha miradi katika maeneo mbalimbali ya visiwa hivyo kushirikisha viongozi wa maeneo husika ili kuepusha hasara ya pesa za wananchi kupotea kiholela.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa CCM Jimbo la Kiembesamaki, Ramadhan Mrisho Rupia, wakati alipofanya ziara ya kukagua mtaro wa maji ya mvua unaotoka Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume hadi Shule Kiembesamaki.

Alisema wamebaini kuwa wanaotengeneza mitaro ni wafanyakazi wa serikali na hawajui kero zinazowapata wananchi katika kipindi cha mvua hivyo wakikaa na viongozi wa chini watajua kero zao.

"Ni jambo la msingi wanapoanzisha miradi kama hii washirikishe uongozi wa sheha na madiwani na wao ndio wanaojua kero zinazowakabili wananchi wa maeneo yao," alibainisha.

Alisema mtaro huo bado haujakidhi mahitaji ya wananchi katika changamoto ya kutuama maji katika jimbo hilo hasa katika kipindi cha mvua ya masika.

"Bado hatukuridhika na hali ya mtaro huu kwani kuna maeneo mengi bado ni kero kwa wananchi wetu katika kutuama maji ya mvua na tunaona kabisa hazijatiliwa nguvu kuondolewa tunasubiri maafa yatokee tuanze kutoa pole," alibainisha.

Alisema zipo njia nyingi za ndani katika Jimbo la Kiembesamaki yanaendelea kujaa maji katika kipindi cha mvua hali ambayo inasababisha wananchi kukosa makazi hasa wale wanaokaa mita 20 hadi 50 ya barabara.

Alisema mradi huo umejikita zaidi kwa barabara na watumiaji wake kuwa salama, lakini serikali haijakaa kuona wanasaidia vipi wananchi hasa katika kipindi cha mvua.

Pia alisema Chama Cha Mapinduzi ndio chama kinachoisimamia serikali kuhakikisha inatekeleza ilani yake kwa vitendo kama ilivyoahidiwa kwa wananchi katika kipindi cha wananchi ikiwamo kuwatatulia kero zao mbalimbali zinazowakabili.

Aliiomba halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB), kusaidia maeneo madogo yanayotuama maji, kusafirisha katika mitaro mkubwa ili kuepusha maafa kwa wananchi ya kujaa maji katika nyumba zao na mali zao.

Diwani wa wadi ya Mbweni, Hafidh Ali Ramadhan, alisema wamekuwa wakipata malalamiko kwa wananchi kuhusu kujaa maji katika maeneo yao na kuomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuwashirikisha katika maeneo yao wanayofanyia kazi ili kutoa maelekezo na wao ndio wanaoahidi wananchi kipindi cha kampeni.

Alisema wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki ni waathirika kwa kipindi kirefu kuhusu kadhia ya maji katika kila msimu wa mvua.

Injinia kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Yussuf Khamis Haji, alisema mradi huo kwa kiasi kikubwa umesaidia Uwanja wa Ndege, lakini bado lipo eneo la mlango wa kuingilia VIP tatizo lipo kwa kuwa inaponyesha mvua maji yanakaa.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mipango kutoka Baraza la Manispaa Magharibi 'B', Ameir Ali Haji, aliahidi kulisimamia suala la usafi wa mitaro hiyo na maeneo ya barabara ili kuona mji unakuwa safi.

## Shule zinazorudisha watoto kwa kukosa sare kukiona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'B', Hamida Mussa Khamis, amezitaka shule zote zilizo chini ya wilaya hiyo kuacha kuwarudisha watoto kwa kisingizio cha kukosa sare.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wazazi, walezi na watoto yatima wa shehia 34 za wilaya hiyo katika Shule ya Urafiki Mwanakwerekwe baada ya kupokea malalamiko ya watoto kurejeshwa Shule kwa kisingizio cha kukosa sare.

Alisema serikali hairuhusu mtoto yeyote hasa yatima kurudishwa shule kwa kisingizio cha kutokuwa na sare na kufanya hivyo ni kumkosesha haki yake ya msingi ya kupata elimu.

"Hakuna shule yoyote yenye mamlaka ya kuzuia watoto ambao hawana sare za shule hasa yatima kutoingia shule na yeyote tutakayembaini amefanya hivyo basi hatua zitachukuliwa," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya amemwagiza mkurugenzi wa elimu wa wilaya hiyo na watendaji wengine wa elimu kulisimamia suala hilo ili kila mtoto anapata haki ya kusoma.

"Jambo hili nisilione wala kulisikia tena naamini kwamba ndani ya wilaya yangu halijawahi kutokea, Mkurugenzi na watu wako jipangeni vizuri kulisimamia hili," alisisitiza.

Alisema serikali imejitahidi kuweka sawa suala la vifaa vya wanafunzi ili kuendeleza dhana ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ya kutoa elimu bure kwa watoto na kuona kila mtoto anapata fursa ya kusoma.

Agizo hilo la Mkuu wa wilaya linatokana na Mjumbe wa bodi ya Step Up Foundation, Sleyum Mustapa Jumbe, kuuomba uongozi wa wilaya hiyo na serikali kwa ujumla kulisimamia suala hilo ili kuruhusu watoto wasiokuwa na sare kuingia shule na changamoto hizo zipo nje ya uwezo wao.

Alisema zipo baadhi ya shule zinazozuia watoto hasa yatima kutoingia shule kwa kisingizio cha kukosa sare hali ambayo inawakosesha kupata elimu kama watoto wengine.



Mwenyekiti wa Kamati ya Wanahabari Zanzibar, Farouk Karim (kushoto), akizungumza jana, kuhusu tuzo za habari, zitakazoshindaniwa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, yatakayofanyika mwezi Mei, mwaka huu katika Chuo cha Habari Kilimani Zanzibar. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Taasisi yaanza utekelezaji sera ya uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao Baharini, imeanza utekelezaji wa sera ya uchumi wa bluu na uvuvi kwa lengo la kuwasaidia wananchi kutumia fursa zilizomo katika sekta hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Ramla Omar, aliyasema hayo baada ya uzinduzi wa uvunaji wa majongoo ya bahari katika shehiya ya Kikungwi na kueleza kuwa ufugaji huo unaweza kuwa wa kibiashara zaidi.Alisema iwapo wafugaji hao watafuga kibiashara watajikwamua na hali ngumu za kimaisha na kupata kipato.

"Wafugaji watajikita zaidi kufuga kibiashara watapata tija zaidi na kupunguza tatizo la ajira kwa wananchi na kufaidika na fursa hiyo katika kujikwamua na umaskini," alisema.

Alisema eneo la Kikungwi lilikuwa limefungwa kwa kipindi kifupi cha mwezi mmoja na wiki mbili kwa shughuli ya ufugaji majongoo kwa ajili ya majaribio ya utafiti na kufunga eneo la Bungi na Kikungwi kwa shughuli hiyo.

Alisema utafiti huo umefanyika mwaka 2019 kwa kulifunga eneo hilo kwa shughuli hiyo kwa ajili ya upatikanaji wa vifaranga vya majongoo ambao utafiti ulionyesha maeneo 18 yalijitokeza Zanzibar na manane kwa Pemba ambayo ni mazuri kwa ufugaji wa majongoo.

Alisema walifunga maeneo hayo Januari 15, mwaka huu na pia walikuwa wanafuatilia kwa ukaribu ukuaji pamoja na maendeleo ya ukuaji wa majongoo hayo kwa ujumla.

Alisema wataendeela kufunga maeneo hayo kwa ajili ya kufuga vifaranga vya kuwapatia wananchi.

Pia taasisi ya utafiti inafanya kazi kwa kushirikiana na Idara ya Maendeelo ya Uvuvi kwa pamoja ili kuona wanawasaidia wananchi ambao wanaoishi karibu na pwani.Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Said Juma Ali, alisema upatikanaji wa majongoo bahari katika pwani ya Shehia ya Kikungwi utasidia kupunguza changamoto ya uhaba wa vifaranga vya majongoo kwa wafugaji.

Kwa upande wa Ofisa Maendeelo ya Uvuvi kitengo cha ufugaji wa mazao ya baharini, Thomas Rafael, alisema zoezi la kuhifadhi majongoo limeanza tangu Januari na wananachi wa Kikungwi wamelifurahia na wamekuwa wabunifu wazuri.

Alisema wananchi wa kijiji hicho wanajivunia kupata majongoo mengi na wamepata mafanikio makubwa, wameshauri kuongeza maeneo mengine ya kufugia ikiwamo maeneo mengine mazuri kwa hifadhi kwa faida yao na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake Katibu wa Kamati ya Uvuvi Shehiya ya Kikungwi, Bahati Issa Suleiman, alisema wanafaidika kilimo cha majongoo hivyo ni faraja kubwa na katika maeneo yanayoingia jongoo wengi ni Shehiya ya Kikungwi.

Alisema wanawake wanafaidika mara mbili zaidi ikiwamo kujiajiri na kuondokana na utegemezi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA A. MAIMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0663/0005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SANGITI SEKONDARI** mwaka 2011. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/170978/2021.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 40 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**DICKSON SHABAN MAKAMBA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**DEBORAH TWAHILU SHEUYA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27th Mwezi wa April 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 30th Mwezi wa March, 2021.

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 31 Mwezi wa MARCH 2021
NAIBU MSAJILI
NAKALA KWA:

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 15/2021**
**MDAI ELIZABETH MICHAEL**

**DHIDI YA**

**MDAIWA ABDALLAH SHAIBU**
**KWA ABDALLAH SHAIBU**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA PESA TASLIM Tsh. 500,000.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 06/04/2021 saa 2:30 asubuhi. Kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 25/03/2021.

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA USHUHUDA WA MALIPO**
**(ACKNOWLEDGEMENT FORM)**

**USHUHUDA YENYE KUMB NA: DMC/LD/25717**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA.**

ARDHI: **KIWANJA NA. 98 KITALU 'F' ENEO LA MAPINDUZI SOUTH YENYE L. O. NO 1027068.**
MUOMBAJI: **SIRI YUSUFU VYAMAGILA WA S.L.P. 23, DODOMA**

**TAARIFA IMETOLEWA**, Kwamba barua ya ushuhuda wa malipo iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa nakala mbadala ya barua hiyo iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya tangazo hili kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

**BARUA YA USHUHUDA WA MALIPO NAKALA HALISI** ikionekana,
Irudishwe kwa Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji,
P. O. BOX 1249,
DODOMA.
Imetolewa

**LEMSI NGOLE**
**AFSA ARDHI**
**DODOMA**
**31/03/2021**

---

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Taasisi ya mikopo ya **IMARIKA FACILITY LIMITED** yenye namba ya usajiri (Incorporation number) **140457434** na **TIN No.140-457-434** ambayo ilikua inatarajia kuanza kuto huduma za mikpo mkoa wa Dar es Salaam. Imeshindwa kuendelea kutoa huduma za mikopo kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo.
Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DORICY TWAIS KALINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.502 CVK.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/RUJ/RB/174295/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/04)**
**Mahakama ya mwanzo**
**KINONDONI**
**Wilaya ya KINONDONI**
**MADAI NAMBARI 252 YA 2020**
**Mimi WINIFRIDA HIGGINS MASSAWE**
**Namdai**
**Mdaiwa BENROSE TANZANIA LTD**
**Kwa BENROSE TANZANIA LTD**
Kwakuwa mdaiwa/mdai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba

**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
**KUSIKILIZA SHAURI LAKO**
Kwahiyo mnahitajiwa/tunahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii ALHAMISI tarehe 06/04/2021 saa 8:30 asubuhi/alasiri kwakujibu madai hayo,na kwakuwa siku hiyo ni aikua ya kukata shauri hilo,ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinanzohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiteteakatika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa na chapa ya mahakama hii leo 01/04/2021.

---

**DABRI AUCTION MART COMPANY LIMITED**
We are dealing with Debt collection, General Auctioneers & Commission Agent
Email: Dabriauctionmart@yahoo.com Website: dabriauctionmart.co.tz P.o.Box 664 Dar es salaam
Location: Mwananyamala Phone: +255 657 507050/ +255 713401175

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Dabri Auction Mart Company Limited** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya Letshego na mamlaka tulionayo kisheria tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana tajwa kama ilivyoorodheshwa hapa chini:

| S/N | JINA LA MKOPAJI | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 110128 KIWANJA NAMBA 249 KITALU NAMBA 6 | KIBADA,MANISPAA YA TEMEKE | TAREHE 06/04/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 121999 KIWANJA NAMBA 135 KITALU NAMBA 32 | BUYUNI,MANISPAA YA ILALA | TAREHE 06/04/2021 SAA 9:00 ALASIRI |

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mnunuzi atalazimika kulipia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14 tangu siku ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipia salio ndani ya siku 14, atakua amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa tena.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakua juu ya mnunuzi.

Kwa maelezo zaidi fika kwenye ofisi zetu zilizopo Mwananyamala au wasiliana nasi kwa namba za simu **0713401175 na 0657507050**

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SA-LAAM.**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA A. MAIMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0663/0005** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SANGITI SEKONDARI** mwaka 2011. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/170978/2021.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 40 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**DICKSON SHABAN MAKAMBA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**DEBORAH TWAHILU SHEUYA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27th Mwezi wa April 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 30th Mwezi wa March, 2021.

NAIBU MSAJILI

NAKALA KWA:

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 15/2021**
**MDAI ELIZABETH MICHAEL**

**DHIDI YA**

**MDAIWA ABDALLAH SHAIBU**
**KWA ABDALLAH SHAIBU**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA PESA TASLIM Tsh. 500,000.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 06/04/2021 saa 2:30 asubuhi. Kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 25/03/2021.

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA USHUHUDA WA MALIPO**
**(ACKNOWLEDGEMENT FORM)**

**USHUHUDA YENYE KUMB NA: DMC/LD/25717**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA.**

ARDHI: **KIWANJA NA. 98 KITALU 'F' ENEO LA MAPINDUZI SOUTH YENYE L. O. NO 1027068.**
MUOMBAJI: **SIRI YUSUFU VYAMAGILA WA S.L.P. 23, DODOMA**

**TAARIFA IMETOLEWA**, Kwamba barua ya ushuhuda wa malipo iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa nakala mbadala ya barua hiyo iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya tangazo hili kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

**BARUA YA USHUHUDA WA MALIPO NAKALA HALISI** ikionekana,
Irudishwe kwa Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji,
P. O. BOX 1249,
DODOMA.
Imetolewa

**LEMSI NGOLE**
**AFSA ARDHI**
**DODOMA**
**31/03/2021**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Taasisi ya mikopo ya **IMARIKA FACILITY LIMITED** yenye namba ya usajili (Incorporation number) **140457434** na **TIN No.140-457-434** ambayo ilikua inatarajia kuanza kuto huduma za mikpo mkoa wa Dar es Salaam. Imeshindwa kuendelea kutoa huduma za mikopo kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo.
Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DORICY TWAIS KALINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.502 CVK.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/RUJ/RB/174295/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/04)**
**Mahakama ya mwanzo**
**KINONDONI**
**Wilaya ya KINONDONI**
**MADAI NAMBARI 252 YA 2020**
**Mimi WINIFRIDA HIGGINS MASSAWE**
**Namdai**
**Mdaiwa BENROSE TANZANIA LTD**
**Kwa BENROSE TANZANIA LTD**
Kwakuwa mdaiwa/mdai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba

**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
**KUSIKILIZA SHAURI LAKO**
Kwahiyo mnahitajiwa/tunahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii ALHAMISI tarehe 06/04/2021 saa 8:30 asubuhi/alasiri kwakujibu madai hayo,na kwakuwa siku hiyo ni aikua ya kukata shauri hilo,ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinanzohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiteteakatika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa na chapa ya mahakama hii leo 01/04/2021.

**DABRI AUCTION MART COMPANY LIMITED**
*We are dealing with Debt collection, General Auctioneers & Commission Agent*
Email: Dabriauctionmart@yahoo.com Website: dabriauctionmart.co.tz P.o.Box 664 Dar es salaam
Location: Mwananyamala Phone: +255 657 507050/ +255 713 401175

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Dabri Auction Mart Company Limited** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya Letshego na mamlaka tulionayo kisheria tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana tajwa kama ilivyoorodheshwa hapa chini:

| S/N | JINA LA MKOPAJI | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 110128 KIWANJA NAMBA 249 KITALU NAMBA 6 | KIBADA,MANISPAA YA TEMEKE | TAREHE 06/04/2021 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 2. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 121999 KIWANJA NAMBA 135 KITALU NAMBA 32 | BUYUNI,MANISPAA YA ILALA | TAREHE 06/04/2021 SAA 9:00 ALASIRI |

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mnunuzi atalazimika kulipia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14 tangu siku ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipia salio ndani ya siku 14, atakua amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa tena.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakua juu ya mnunuzi.

Kwa maelezo zaidi fika kwenye ofisi zetu zilizopo Mwananyamala au wasiliana nasi kwa namba za simu **0713401175 na 0657507050**

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Suu Kyi afikishwa mahakamani

**Yangon,** MYANMAR

WAKILI wa kiongozi wa Myanmar, aliyepinduliwa Aung San Suu Kyi, ameliambia Shirika la Habari la Reuters kuwa, kiongozi huyo hajawekewa mashtaka mapya baada ya kufikishwa mahakamani jana.

Kauli hiyo inakuja wakati mjumbe wa Umoja wa Mataifa (UN), kutahadharisha kuwa Myanmar iko katika hatari ya kutumbukia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe.



Suu Kyi anakabiliwa na mashtaka kadhaa ya uhalifu ambayo huenda yakampelekea kufungiwa maisha kuwania nafasi ya uongozi.

Mawakili wake walifanya mkutano wa kwanza pamoja naye, kupitia njia ya video katika kituo cha polisi, tangu alipozuiliwa na jeshi Februari Mosi.

Suu Kyi (75), hajaonekana hadharani tangu wakati huo, ingawa mawakili wake wanasema alionekana mwenye afya njema, licha ya kuwa kizuizini kwa miezi miwili. **DW**

## Uchaguzi wakwama Somalia

**New York,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, limeelezea wasiwasi wake juu ya mgogoro wa kisiasa nchini Somalia, kuhusu kufanyika kwa uchaguzi mpya.

Mkuu wa Sera ya Marekani katika Umoja wa Mataifa, alisema.

Muhula wa miaka minne wa Rais Mohamed Abdullahi Mohamed, ulimalizika mwezi uliopita bila kuteuliwa mrithi wake.

Bunge la Somalia, lilitarajia kuchagua rais mpya Februari 8, ingawa uchaguzi ulicheleweshwa na wabunge wapya hawajachaguliwa.

Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa (UN), Linda Thomas-Greenfield alisema wajumbe 15 wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wamekaribisha juhudi zilizofanywa kupata makubaliano kati ya viongozi wa serikali ya shirikisho la Somalia na majimbo ya shirikisho.

"Wameelezea wasiwasi wao juu ya mvutano wa kisiasa na wakatoa wito kwa viongozi wa Somalia kushiriki mazungumzo, bila masharti yoyote, ili kutatua masuala yaliyosalia," alisema. **RFI**

# Niger yachunguza jaribio la mapinduzi

**Niamey,** NIGER

MAMLAKA nchini Niger imebaini kwamba jaribio la mapinduzi, saa 48 kabla ya kuapishwa kwa rais mpya wa Jamhuri.

Kulingana na vyanzo rasmi, angalau wanajeshi 15 walikamatwa kwa ajili ya uchunguzi.

Jaribio hilo lilitibulia usiku wa Jumanne kuamkia Jumatano Machi 31, mwaka huu mjini Niamey.

Wakazi wa mji mkuu waliamshwa asubuhi na milio ya risasi na zana nzito nzito za kijeshi, makabiliano yaliyodumu nusu saa karibu na makazi ya rais.

**Kulingana na vyanzo rasmi, angalau wanajeshi 15 walikamatwa kwa ajili ya uchunguzi.**

Kiongozi wa washambuliaji, Kapteni Gourouza anasemekana yuko mafichoni na ndiye mtu anayetafutwa sana nchini humo.

Askari waliokamatwa wakati wa shambulio na wengine waliokamatwa mahali pengine inasemekana wamekubali kuwa, walishiriki katika jaribio hilo chini ya maagizo ya Kapteni Gourouza.

Ofisa huyo wa jeshi la anga ambaye, kulingana na vyanzo vingine, alifanikiwa kuvuka mji wa Niamey kutoka Mashariki kuelekea Magharibi, hadi karibu na makazi ya rais, akiwa na silaha nzito bila kuonekana wala kukamatwa.

"Tumewaona wakija wiki chache zilizopita, kimethibitisha chanzo cha usalama cha ngazi ya juu, tumewakamata wakitaka kufanya uhalifu wao, waliwapiga risasi askari wetu, " chanzo hicho kilisema.

Gourouza, ambaye picha zake ziko kwenye mitandao ya kijamii, ndiye mtu anayetafutwa na Idara zote za ujasusi zinaendelea na operesheni ya kumsaka. **RFI**



Vikosi vya usalama nchini Afghanstan wakiwa wamembeba mwathiriwa wa bomu lililopigwa eneo la Kamar Kalagh, jana. Polisi wawili waliuawa kutokana na shambulio hilo karibu na kituo cha ukaguzi cha polisi kando ya barabara ya mkoa wa Herat. **PICHA: XINHUA**

# Madagascar yakubali chanjo corona

**Antananarivo,** MADAGASCAR

MADAGASCAR imeamua kubadili mtazamo wake juu ya kukabiliana na virusi vya corona na kujumuika na jitihada za kimataifa kupata chanjo ya corona.

"Kuna hatua kadhaa ambazo inabidi kupitia kabla ya kupata chanjo hiyo, lakini kujisajili ndio jambo la msingi na hatua muhimu kabla ya kupata chanjo hiyo.

"Tayari tuko kwenye hatua muhimu katika usajili," Waziri wa Afya, Prof. Jean Louis Rakotovao alisema kwenye video aliyoiweka kwenye ukurasa wa wizara yake wa Facebook.

Awali Madagascar ilionyesha kutokuwa na nia ya kushiriki katika jitihada za kupokea chanjo. Ilidai kuwa ni bora kutumia dawa ya asili inayofahamika kama Covid-Organics.

Dawa hiyo ambayo iko katika mfumo wa chai au vidonge, ilitangazwa na Rais wa taifa hilo, Andry Rajoelina, kwamba ndio dawa ya corona.

Hata hivyo hakuna tiba ya virusi vya corona, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO). **BBC**

## Navalny agoma kula

**Moscow,** URUSI

MKOSOAJI wa serikali ya Urusi, ambaye yuko gerezani, Alexei Navalny amesema kuwa ataanza mgomo wa kula kushinikiza kupewa huduma bora za matibabu kufuatia maumivu makali ya mgongoni na miguu kufa ganzi.

Kwenye ujumbe alioandika katika ukurasa wake wa Instagram juzi, Navalny (44), alisema ameanza mgomo wa kula kutaka sheria iheshimiwe na daktari aruhusiwe kumtembelea gerezani. Navalny alilalamika kwamba amepewa dawa za kupunguza maumivu, ingawa hajafanyiwa vipimo ipasavyo. **DW**

# FATI ADOKEZA KUKAA NJE YA DIMBA MWAKA




**BARCELONA,** Hispania

KINDA wa Barcelona, Ansu Fati amedokeza anaonekana anaweza kuwa nje ya dimba kwa mwaka mmoja kutokana na majeruhi yake ya sasa ya goti.

Fati aliumia vibaya goti Novemba, mwaka jana, akiwa amecheza mechi 10 kwenye mashindano yote na kufunga mabao matano.

Winga huyo wa Hispania alifanyiwa upasuaji na iliripotiwa kwamba angekaa nje kwa muda wa miezi minne na Aprili hii angekuwa uwanjani, lakini sasa kurudi kwake dimbani kumesogezwa mbele, huku kukiwa hakuna muda maalumu uliotajwa wa kurudi uwanjani.

Hii sio mara ya kwanza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kuwa majeruhi kwa muda mrefu, kwani Fati amebainisha aliwahi kukaa nje ya dimba karibu mwaka mmoja akijiuguza.

"Miaka michache iliyopita niliumia vibaya, sikuweza kucheza kwa zaidi ya mwaka mmoja," aliandika Fati kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Kulikuwa na siku nyingi za maumivu, lakini kujifunza mambo mengi. Ilinisaidia mimi kukubaliana na hali halisi. "Pamoja na familia yangu na wataalamu walinisaidia wakati ule, niliahidi kuendelea kujituma zaidi kufanya kile ninachokipenda zaidi, kucheza soka.

"Bahati mbaya, sasa naona tena nipo kwenye hali kama ile, nikikabiliwa na wakati sawa na ule.

"Naona kwamba naweza kuwa nje ya dimba kwa mwaka mzima, kwani hali yangu bado sio shwari kwa sasa."

# Torres aziingiza vitani Real Madrid, Man United

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perezameripotiwa kukasirika baada ya Manchester United kujitosa kwenye mbio za kumfukuzia beki wa Villarreal, Pau Torres.

Beki huyo amekuwa akisakwa na timu nyingi za Ulaya kuelekea dirisha lijalo la uhamisho wa majira ya joto, huku kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer akiamini atakwenda kunasa huduma yake ili akacheze sambamba na Harry Maguire.

Solskjaer anatafuta beki wa kati anayetumia mguu wa kushoto na Torres anafiti kwenye mpango wa kocha huyo, jambo linaloweka uwezekano mkubwa akaenda kukipiga United msimu ujao.

Na jambo hilo sasa limemuibua Perez ambaye sasa amepanga kufanya kila linalowezekana kumsajili nyota huyo.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, Perez anaona kwamba, Torres anafaa zaidi kwenye kikosi chake, hasa wakati huku kukiwa na sintofahamu ya majaliwa ya nahodha wa kikosi chao, Sergio Ramos.

Ripoti ya gazeti hilo imebainisha kwamba, Perez kwa sasa amejipanga kuingia kwenye vita hiyo na kuhakikisha Torres anakuwa mali yao wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo, Torres pia anawaniwa na klabu za Chelsea, PSG, hasa baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kule Villarreal.




# Haaland aandaliwa mshahara kufuru




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inahitaji kumlipa, Erling Haaland mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki kama wataamua kukamilisha dili la kumsajili nyota huyo wa Borussia Dortmund kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa The Sun.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 ni mmoja wa wachezaji wanaotazamwa zaidi ulimwenguni kuelekea dirisha la uhamisho la msimu unaokuja wa joto, na amekuwa akihusishwa zaidi na kikosi hicho cha Pep Guardiola na klabu nyingine kama Manchester United, Chelsea, Real Madrid na Barcelona.

Kwa mujibu wa The Sun, Dortmund wanamtaja Haaland kuwa na thamani ya karibu euro milioni 150, wakati nyota huyo akihitaji mkataba wa kumlipa pauni 600,000 kwa wiki.

Na hilo litamfanya kuwa mchezaji atakayelipwa mshahara mkubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu England. Haaland amecheza mechi 31 kwenye michuano yote akiwa na Dortmund, akifunga mabao 33 na kutoa pasi za mwisho nane.

Kama City watashindwa kufikia makubaliano ya masharti anayohitaji nyota huyo, basi watalazimika kupata mbadala wake, ambaye anatajwa kuwa ni Harry Kane wa Tottenham Hotspur, ambaye ameripotiwa kwa sasa anafikiria kutafuta changamoto mpya.

HABARI MICHEZO

# Madrid yampa Ramos mwaka mmoja

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kumwaandalia ofa ya mkataba wa mwaka mmoja tu beki wao wa kati, Sergio Ramos ili aendelee kukipiga hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Nahodha huyo wa Real Madrid mkataba wake wa sasa unamalizika Juni, mwaka huu na bado hakujawa na uhakika kuhusu majaliwa yake.


Ingawa Real Madrid imeonyesha kuwa inahitaj kumbakisha nahodha huyo wa timu ya taifa ya Hispania, lakini ofa ya mkataba mmoja inaweza kuwa kikwazo.

Kutokana na umri wake wa miaka 35, ni wazi kwamba, Ramos hataweza kukubali kusaini mkataba wa mwaka mmoja tu kuitumikia klabu hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania, Ramos mwenyewe anataka mkataba angalau wa miaka miwili na mshahara mnono, ili aweze kumalizia soka lake hapo.

Ramos pia anatajwa kuwaniwa na klabu za Manchester United, Tottenham Hotspur na Paris Saint-Germain.

Miamba hiyo ya soka la Hispania, pia imefungua milango ya kumnasa, David Alaba kutoka Bayern Munich kama mbadala wa Ramos kama ataondoka.






# LOW ATAJWA KUMRITHI ZIDANE

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wameripotiwa wapo sokoni kusaka mrithi wa Kocha, Zinedine Zidane, huku gwiji wa klabu hiyo Raul na bosi wa sasa wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joachim Low wakiongoza kwenye orodha.

Zidane anaendelea kuwa mwenye msukumo mkubwa pale kwenye Uwanja wa Bernabeu baada ya kuwa na msimu mgumu.

Zidane kwa sasa anahitaji taji moja na ikiwa atashindwa kulipata basi atakuwa kwenye hati hati ya kutimuliwa klabuni hapo.

Chanzo kimoja cha habari cha nchini Hispania kimelidokeza gazeti la AS kwamba, tayari klabu imeshaweka mipango mezani ya kumpata mrithi wa Zinedine.

Low, ambaye ana uzoefu mkubwa wa takribani miaka 15 anatarajia kuachia ngazi kama kocha wa Ujerumani msimu wa majira ya joto unaokuja na anatajwa kuongoza kwenye orodha ya wanaohitajika kule Madrid.

Kuna taarifa zilizothibitishwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 61 kuwa amekuwa akijifunza lugha wa Kihispania.

Raul, mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid pia anatajwa kuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata kibarua hicho kama Zidane atatimuliwa.

# *Willian: Arteta ataivusha Arsenal*

**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal, Willian amesema kuwa anaamini kikosi hicho kitarudi kwenye ubora wake chini ya kocha wake mkuu, Mikel Arteta.

Willian ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Brazil, amebainisha kuwa anaamini timu hiyo ipo mikono salama chini ya Arteta na itatamba kwa mara nyingine tena.

Ikumbukwe Arsenal haijashinda ubingwa wa Ligi Kuu England tangu mwaka 2004 na kwa sasa haina uhakika wa kufanya hivyo, kwa sababu inashika nafasi ya 10 kwenye msimamo.

Kiungo huyo amesema wapo kwenye mwendo mzuri chini ya msaidizi huyo wa zamani wa Pep Guardiola kule Manchester City.

"Nadhani ana kila kitu cha kuifanya iwe na dira nzuri ni klabu kubwa ipo mikono ya kocha bora ana kila kitu kitakachoifanya timu iwe bora," alisema Willian akinukuliwa na Sky Sport.

Willian alijiunga na Arsenal kwa mkataba wa miaka miwili akitokea kwa majirani zao wa jiji la London, Chelsea.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: SITALIPA KISASI KWA RAMOS

## Ni kutokana na beki huyo kumuumiza kwa makusudi wakati timu zao zilipokutana...

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesema hana haja ya kulipa kisasi kwa beki, Sergio Ramos wakati timu yake ya Liverpool itakapokutana na Real Madrid kwenye mchezo wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Liverpool watacheza na Madrid Jumanne ya Aprili 6, mwaka huu, mchezo ambao utakumbushia fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19, wakati timu hizo zilipokutana.**

Kwenye mchezo huo, Salah aliumizwa na Ramos dakika za awali na kulazimika kutolewa nje ya dimba na Real Madrid wakalibeba taji hilo.

Na sasa wakati kukiwa na presha kubwa kwa mashabiki pamoja na wachezaji wa timu zote mbili kuelekea mechi hiyo, Salah amesema wapo tayari kushinda licha ya ukweli kwamba mchezo huo utakuwa mgumu, kwani Real Madrid wana kikosi kizuri.

Alipoulizwa na Marca kama anahofia kukutana na nahodha wa Madrid, Ramos Salah alijibu; "Huo ni ni mchezo uliopita na wala siuwazii, ninachowaza ni kuhusu timu yangu na kila mmoja anawaza hilo na anataka kushinda.

"Ndio hilo tu. Kuhusu kushinda na si vinginevyo.

"Wengi wanafikiri kuhusu kulipa kisasi, hapana, sina haja ya kufanya hivyo kwa sababu ile ilikuwa sehemu ya mchezo tu."

Salah pia alielezea namna ambavyo anawakubali wachezaji kadhaa wa Real Madrid akiwataja Eden Hazard na Luca Modric.

Alipoulizwa kama siku moja anatamani kucheza kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Salah alijibu; "Ndiyo, siku moja inawezekana."

Mara ya mwisho Liverpool walipokutana na Real Madrid katika fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2018 kule Kiev, Salah alilazimika kutolewa nje baada ya kuumia bega kwa kuchezewa vibaya na Ramos.

Tukio hilo lilizua vitu vingi ambavyo vilieleza kuwa nahodha huyo alifanya hivyo ili kupunguza makali ya Liverpool ambao walimtegemea sana Salah kipindi hicho.

## ZISIKUPITE

### MESSI, HAALAND KUMEKUCHA

MANCHESTER City inafuatilia kwa karibu kuwasajili mshambuliaji wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi, 33, pamoja na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland (20). ***(Sun)***

### DYBALA KUMPISHA POGBA

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba (27), huenda akaondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu, huku Juventus ikiwania kumsajili na pia kumuuza mshambuliaji wake, Paulo Dybala mwenye miaka 27, katika makubaliano ya mabadilishano. ***(Tuttosport)***

### SPURS: KANE HAUZWI

KLABU ya Tottenham Hotspur ina imani kubwa kwamba, itaendelea kuwa na Harry Kane (27), na wala haina mpango wa kumuuza katika klabu nyingine ya Ligi Kuu England. Manchester City na Manchester United zinatajwa kumnyatia. ***(Manchester Evening News)***

### BAYERN YAMWANIA SON

BAYERN Munich inawania kumsajili mshambuliaji wa Tottenham, Son Heung-min, 28, na iko tayari kumsubiri mchezaji huyo wa Korea Kusini ambaye mkataba wake unamalizika 2023. ***(Football Insider)***

### DONNARUMMA AGOMBEWA

CHELSEA, Manchester United, Juventus na Real Madrid bado zinamfuatilia golikipa wa Italia, Gianluigi Donnarumma, 22, ambaye amekataa ofa mbili za mkataba mpya pale AC Milan. ***(Gianluca di Marzio, via Mail)***

### WIJNALDUM SAFI

BARCELONA inaonekana kuwa yenye uwezekano mkubwa wa kumsajili, Georginio Wijnaldum, 30, ambaye mkataba wake na Liverpool unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Marca)***

### TOWNSEND MAMBO MAGUMU

WINGA wa Crystal Palace, Andros Townsend (29), amesema kuwa klabu hiyo imemwarifu yeye pamoja na wachezaji wengine ambao mikataba yao inamalizika, hatima zao hazitajadiliwa hadi mwisho wa msimu. ***(Talksport)***

### AGUERO ATAFITI JUVE

MSHAMBULIAJI Sergio Aguero, 32, atakuwa "bora" zaidi akisajiliwa Juventus, amesema gwiji wa klabu hiyo ya Italia, Franco Causio. ***(Gazzetta Dello Sport, via Goal)***

### RODRIGO AFUNGUKA

STRAIKA wa Leeds United, Rodrigo, 30, ametupilia mbali uvumi kuwa hana furaha Elland Road baada ya kuripotiwa anataka kurudi Ligi Kuu Hispania. ***(Leeds Live)***

### TEVEZ ANUKIA MLS

MSHAMBULIAJI wa Boca Juniors, Carlos Tevez, 37, ambaye ana miezi 12 kuamua kama ataendeleza mkataba wake na mabingwa hao wa Argentina baada ya msimu huu, anahusishwa na kuhamia Marekani. ***(ESPN)***

## Polisi kuichezesha gwaride Biashara

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Polisi Tanzania limesema liko tayari kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa Aprili 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume Musoma mkoani Mara.

Kikosi hicho sasa hivi kinaendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushiriki kilichoko Moshi, Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini alisema wachezaji wake wote wako fiti na wanausubiri mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na rekodi ya wenyeji wao wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Malale alisema matarajio pekee aliyonayo katika mchezo huo ni kuondoka na pointi tatu na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo itakayomalizika ifikapo Julai 11, mwaka huu.

"Maandalizi yanaendelea vizuri na hatuna wasiwasi, wachezaji wote wanaendelea kujifua ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Malale.

Kocha huyo aliongeza ametumia muda wa mapumziko kuyafanyia kazi makosa madogo madogo ambayo aliyabaini sasa nyota wake wamejengeka na wako tayari kwa ajili ya kupambana.

## Michuano ya U-21 netiboli yaandaliwa

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimeitaka mikoa kuandaa timu zao kwa ajili ya kushiriki mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ambayo yatafanyika hivi karibuni, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, alisema kila mkoa unatakiwa kuendesha mashindano katika ngazi yake ili kujiweka tayari na michuano ya taifa.

"Tunatarajia kuwa na mashindano ya vijana mwezi huu, baada ya kumalizika kwa maombelezo nitawajulisha zaidi kila kitu kinachoendelea," alisema Devotha.

Alisema viongozi wa mikoa wamemthibitisha kushiriki mashindano hayo ambayo yatasaidia kuibua vipaji vipya.

"Kalenda yetu ya mwaka huu inaonyesha tutakuwa na mashindano mbalimbali, kwa sasa tutaanza na vijana halafu hapo baadaye tutaandaa michuano mengine na tutawatangazia ni mashindano yapi yanafuata," Devotha alisema.

# TFF, KLABU ZAMPONGEZA NA KUMKARIBISHA GEKUL

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetoa salamu za pongezi kwa Pauline Gekul ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alitangaza Baraza la Mawaziri juzi katika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma, na kumtaja Gekul ataungana na Waziri Innocent Bashungwa katika wizara hiyo.**

Katika salamu za pongezi, TFF imesema inamtakiwa kila la kheri Gekul katika kutekeleza majukumu yake na inaahidi kutoa ushirikiano kwa kiongozi huyo.

"Hongera, tunakutakia kila la kheri katika majukumu yako mapya," ilisema kwa kifupi taarifa ya TFF.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema klabu hiyo inampongeza Gekul na inafahamu ni mmoja wa watendaji wazuri na hawana shaka naye.

"Tunamkaribisha na tayari tumeshaandika barua ya pongezi, kuanzia leo (jana), wakati wowote anaweza kuipata ofisini kwake Dodoma na tunamtakia kila la kheri na majukumu yake mapya, tumefurahi pia kupata tena waziri mwanamke kama ilivyokuwa kwa awamu iliyopita tulivyokuwa na Juliana Shonza," alisema Bumbuli.

Kwa upande wa Azam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, alisema yeye binafsi pamoja na klabu yake wanampongeza Gekul na wanamshukuru Naibu Waziri aliyeondoka, Abdallah Uledi ambaye walifanya naye kazi vizuri japo ni kwa muda mfupi.

"Tunampongeza na tunamkaribisha, tunamwambia tutampa ushirikiano na lengo ni kupata mafanikio katika sekta ya michezo, hususani mpira wa miguu," alisema Zacharia.

Kiongozi huyo alisema mara nyingi mawaziri wanawake kwenye wizara hiyo wamekuwa wapambanaji mno ambapo alikumbushia enzi za Fatma Said Ally ambaye alihudumu katika kipindi cha katikati ya miaka ya 1980 ilipojulikana kama Wizara ya Utamaduni wa Taifa, Vijana na Michezo.

"Mama yule (Fatma), alipambana sana kwa kiasi kikubwa hata kuutatua mgogoro mkubwa wa Yanga Ukuta na Yanga Katiba ulipopamba moto wakati huo, lakini namkumbuka mama mwingine, Dk. Fenella Mukangara ambaye naye alikuja kuwa waziri wa michezo, ndiyo maana nasema wanawake wana historia nzuri kwenye michezo." Alisema Zacharia.

Gekul amechukua nafasi ya Ulega ambaye amehamishwa kwenda kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi.



Mchezaji wa bao, Ally Said (kulia), akipambana na Salum Mponda katika mchezo huo kama walivyokutwa wakiwa kwenye eneo la Temeke jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Klabu Ligi Kuu Zanzibar kukutana*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Zanzibar (ZBL), inatarajia kukutana na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Visiwani hapa kesho kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali kuhusiana na mechi za ligi hiyo zilizosalia, imeelezwa.

Kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar imebakisha mizunguko mitano na ili kukamilisha msimu wa 2020/21.

Awali ligi hiyo ilipangwa kumalizika mapema April 12, mwaka huu, lakini ililazimika kusimama ili kupisha kipindi hiki cha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa ZBL, Sheha Mohammed, alisema viongozi wa timu zote wanatakiwa kufika katika kikao hicho kitakachofanyika kwenye ukumbi wa mikutano uliopo katika Uwanja wa Amaan.

Sheha alisema lengo la kikao hicho ni kujadiliana kwa pamoja juu ya namna kumaliza michezo iliyobakia kabla ya kuanza kwa mwezi wa Ramadhani.

"Tutakutana na vilabu ili tuone na wao watatoa mawazo gani katika kuelekea kumaliza msimu kabla ya kuingia Ramadhani, mpaka sasa tumebakisha wiki moja na kama tukisema tuendelee na ligi ndani ya wiki moja hatuwezi kumaliza mizunguko yote, hivyo tutawasikiliza maoni yao halafu baadaye tutatoa taarifa rasmi," alisema Sheha.

Kwa kawaida ligi zote za Zanzibar husimama katika kipindi cha Ramadhani ili kupisha ibada ya funga ambayo iko katika nguzo za dini ya kiislamu.

Michezo

Ijumaa Aprili 2, 2021

Nipashe



Salah: Sitalipa kisasi kwa Ramos UKURASA 22



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi chini ya usimamizi wa Kocha wa Viungo, Adel Zrane (kulia), kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: SSC**

# MANULA AIWEKA SIMBA MTEGONI

## Ni kuhusu uamuzi wa kumuuza, mashabiki...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na mabingwa wa Ligi Kuu Sudan, klabu ya Al Mereikh, golikipa chaguo la kwanza la Wekundu wa Msimbazi, Aishi Manula amesema hatima kuhusu 'dili' hilo ameliacha mikononi mwa viongozi wa klabu yake.

**Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam hivi karibuni zinasema vigogo hao wa Sudan wanadaiwa kutenga kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 200 ili kumsajili golikipa huyo ambaye ni mlinda mlango namba moja wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars).**

Akizungumza na gazeti hili jana, Manula alisema yeye bado ni mchezaji mwenye mkataba na Simba, hivyo atasikiliza na kufuata uamuzi utakaofanywa na klabu yake hiyo ambayo kwa sasa imeweka mguu mmoja ndani kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Manula alisema mpaka sasa klabu tano zinazoshiriki ligi mbalimbali zimeonyesha nia ya kuhitaji huduma yake, lakini hawezi kuziweka wazi kwa sababu yuko ndani ya mkataba na Simba.

"Kwa sasa ninawasikiliza waajiri wangu ambao ni Simba, kuhusu suala zima la ofa hiyo kwenda au kuendelea kusaidia timu katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Manula ambaye alitua Simba akitokea Azam FC.

"Simba wao ndio wenye nafasi ya kufanya uamuzi wa kuniuza au kunibakiza kwa kuendelea kuitumikia klabu yao, kwangu ni bora kwa sababu nina imani ya kuwa bora zaidi, watakapochukuwa uamuzi wa kuniuza pia itakuwa jambo nzuri kutokana na kupata maslahi kwao na kwangu pia," alisema Manula.

Kuhusu kiwango bora ambacho amekionyesha katika siku za hivi karibuni alisema hizo ni juhudi zake binafsi, mafundisho kutoka kwa kocha wao mpya wa magolikipa Mbrazili Milton Nienov pamoja na ubora wa sasa kikosi hicho cha Simba.

"Simba kwa sasa ni timu bora pia ujio wa kocha Milton umechangia kwa kiasi kikubwa kuwa katika bora, pamoja na makipa wenzangu kwa sababu ukiangalia katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika sisi tuna 'clean sheet nne', tatu zangu na moja ya Beno Kakolanya," Manula alisema.

Manula ambaye msimu uliopita alitangazwa kuwa Kipa Bora ameiongoza Simba kufikisha pointi 10 na kuwa kinara wa Kundi A katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo walishinda bao 1-0 ugenini dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) halafu wakapata ushindi kama huo walipowakaribisha vigogo wa Afrika, Al Ahly kutoka Misri.

Wakati huo huo, kikosi cha AS Vita kikiwa na wachezaji 24 na viongozi tisa kiliwasili nchini jana usiku tayari kwa mchezo wa raundi ya tano utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu aliliambia gazeti hili wachezaji, Meddie Kagere na Luis Miquissone walitarajiwa kurejea nchini jana kuungana na wenzao kwa ajili ya mchezo huo ambao mashabiki 10,000 wameruhusiwa kushuhudia mtanange huo.

## Yanga yawaza pointi 12 Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi amesema mikakati ya kuhakikisha wanashinda michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa ndani ya mwezi huu ili kuendelea kujiimarisha kwenye uongozi wa ligi hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 50, na ratiba inaonyesha wataendelea na kampeni ya kusaka ubingwa kwa kucheza dhidi ya KMC FC ifikapo Aprili 10 halafu Aprili 17 watawakaribisha Biashara United huku Aprili 24 wakiivaa Gwambina na watamaliza mwezi kwa kuikabili Azam FC Aprili 25, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema wanaendelea kufanya mazoezi ili kuhakikisha wanajiweka katika nafasi nzuri ya 'kuchanga karata' zao vizuri na hatimaye kukusanya pointi 12 za awali.

Mwambusi alisema ana matumaini makubwa watafanya vyema kwa sababu kikosi chao kimekamilika baada ya wachezaji wao waliokuwa majeruhi akiwamo Saidi Ntibanzonkiza na Fiston Abdul Razack afya zao kuimarika.

"Hali ya kikosi kilichokuwapo kambini kipo sawa kwa wachezaji waliosalia kambini huku bado Saido na Mukoko Tonombe ambao watarejea mapema wakitokea kwenye majukumu ya timu zao za taifa, tunaendelea na programu ili kuhakikisha tunafikia malengo kwa kuanza kukusanya pointi kwenye mechi hizi nne za mwezi huu," alisema Mwambusi.

Aliongeza baada ya nyota hao kurejea kikosi chake kitaendelea kupambana ili kutoa 'dozi' katika kila mechi watakayocheza ingawa wanafahamu kila mchezo utakuwa na ushindani.

Aliongeza wanajipanga pia kufanya vizuri katika mchezo wao wa hatua ya 16 Bora wa mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga, Rukwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >